# Ratiba ya kipindi cha Ufalme wa Mungu cha Ufuasi

**Toleo la 1**



Kipindi cha Ufalme wa Mungu cha ufuasi ni safari ya ugunduzi inayokupa nafasi ya kupata ufahamu wa utukufu wa Bwana kwa njia kuu, kujua na kuhisi upendo wake  mkuu, kuishi katika nguvu zake za kubadilisha na kujazwa na ukuu wake mkuu. Kutokana na haya, kupata  nguvu za kuwawezesha wengine kujua na kumhusu Mungu na ufalme wake.

Hakimiliki 2015. Kwa nakala za bure tembelea tovuti  www.jesuslovestheworld.info  ama barua pepe info@jesuslovestheworld.info

Upendo wa Mungu ulioonyeshwa katika Yesu, unakamilika tunapojua na kuhisi kuishi ndani yake. Yesu anapenda : ulimwengu upo kuhubiri, kufunza na kutoa mafunzo kuhusu ufalme wa Mungu, ili wote walio tayari waweze kupata msingi katika ukweli wake, ulio katika mzizizi ya upendo wake na kujazwa na ukuu wake.

# Yaliyomo


Mwanzo.......................................................2

1: Kuona kisichoonekana...................................3

2: Kumjua YEYE.................................................4

3: Kujionyesha kwa ubinafsi..............................7

4: Wakati ni sasa.............................................10

5: Mungu aliupenda.......................................13

6: Upendo wa Baba.........................................17

7: Upendo wa Mwana.....................................20

8: Upendo wa Roho Mtakatifu.........................22

9: Kukubaliwa jinsi nilivyo...............................24

10: Kitambulisho - Uzao wa Roho.....................27

11: Kukubalika katika aliyependwa...................32

12: Mahusiano.................................................36

13: Kuwakubali wengine jinsi walivyo...............39

14: Mahusiano – Kuwa sawa.............................42

15: Mahusiano – Ufuasi...................................45

16: Mahusiano - Ufalme wa Mungu..................47

Maombi.......................................................49

10 Daftari za mbegu...................................45

# Mwanzo

*Mungu hufanya kila kitu kutokana na upendo wa kusamehe, kurejesha na kuleta upya mambo yote kwake. Ana uhusiano, uwepo wa karibu na ushirika wa ana kwa ana.*

Ili kila mtu apate mambo ya kutosha kutoka kwa mafunzo haya, nakuuliza:

- tarajia kusikia kutoka kwake Mungu.
- uliza maswali
- yaseme mawazo yako na ujadili.
- andika majibu yako katika makaratasi
- na zaidi ya yote, furahia safari.

## Mpango wa Mungu

Mpango wa wokovu wa Mungu, uliopangwa hapo awali ni kuleta kila kitu, mbinguni na katika ardhi, katika Yesu Kristo, chini ya utawala na uongozi wake.

Mungu katika Yesu Kristo hurejesha uwiano na amani katika ulimwengu. Ndani Yake, tupamoja naye

**Waefeso 1:9-10** *...akiisha tujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa na Uradhi wake alioukusudia katika yeye huyo. Yaani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu va mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam, katika yeye huyo.(NKJV)*

## Kuwafanya Wafuasi

Yesu aliwapa wafuasi wake mamlaka yake ili wanapoendelea na safari ya maisha kupitia Roho wake 'wangewafanya wafuwasi'.

**Mathayo 28:18-20** *Yesu akaja kwao,akasema nao,akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi,enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wafuasi, mikwabatiza kwa jina la Baba na Mwana, na Roho Mtakatifu na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari." Amen. (SUV )*

Ufuasi huanza kwa kumjua Mungu na upendo wake kwako, kwa kumjua yeye ni nani, kile ambacho anafanya na atakachofanya. Kuwa na wakati naye katika uwepo wake, kusikia au kusoma neno lake, katika ibaada, maombi na kushiriki na waumini wengine hutusaidia kumjua.

Tunapoendelea katika mpango huu wa ufuasi, ni ombi langu katika jina la Yesu kwamba kwa Roho wake, utapata ufahamu mkuu wa utukufu wa Bwana na upendo wake mkuu kwako, na utajazwa kwa kiwango cha ukuu wa Mungu, ili ulimwengu uweze kumjua. Amen.

# Awamu ya  1: Kuona Kisichoonekana

*Mungu muumba ana uhusiano. Neno lake ni la kibinafsi.*

*Uwepo wake ni wa karibu. Uumbaji wake ni wa ushuhuda.*

## Maombi ya kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni wimbo mmoja au mbili za ibada ambazo zinatangaza azma ya Mungu ya kujionyesha kwetu.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili kuhusu njia tofauti ambazo Mungu hujionyesha kwetu.  Andika majibu yako katika daftari yako.

Soma **Zaburi 19:1-6, Warumi 1:20,**

Soma **Hosea 12:10 na**

Soma **Mwanzo 31:11**

Mungu hujionyesha wetu kwa njia ya kuumba [ikiwemo hali ya maumbile kupitia kwa

neno la manabii wake na  malaika wa Mungu

Soma **Kumbukumbu la Torati 4:35-39,**

Soma **Mwanzo 15:1, Wafalme wa Pili 5:1, Wafalme wa Pili 5:14-15 na  Yohana 9:1-7**

Mungu anajionyesha kwetu kupitia kwa miunjiza. [ zikiwemo ishara, miujiza, maono na uponyaji]

Soma **Luka 24:27, Yohana 20:31 na  Zaburi 33:6-9**

Mungu anajionyesha kwetu kupitia kwa neno lake. [ikiwemo la kuandikwa na la kunenwa]

Soma **Yohana 1:14-18, 14:6-7 na  Waebrania 1:1-4**

Mungu ajionyesha kwetu kupitia kwa Yesu.

Soma **Yohana 16:13-15 na Yohana wa Kwanza 5:6**

Mungu ajionyesha kwetu kupitia kwa Roho wake.

## Shuhudia

Muulize kila mmoja aseme kwa sentensi mbili au tatu kuhusu jinsi ambavyo Mungu amejionyesha kwao.

## Maombi ya kufunga ya Shukrani

Muulize mtu mmoja amshukuru Mungu kwamba anataka kujionyesha kwetu.

# Awamu ya 2: Kumjua Yeye

*Mungu Muumba anapita mipaka ya wakati na anga, ilhali anajionyesha kibinafsi kwa wakati wetu na anga tuliyomo.*

## Maombi ya Kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni wimbo moja au mbili za kutangaza ukuu wa Mungu.

## Utangulizi

Katika somo la kwanza,tulijifunza njia tofauti ambazo Mungu hujitambulisha kwetu. Tunaposoma Bibilia—Barua ya kibinafsi ya upendo wa Mungu kwetu—twajifunza mengi kumhusu. Hata maneno ya kwanza, '*Hapo mwanzo,Mungu aliumba...*' yatuonyesha kwamba, vyovyote na popote mwanzo ulipokuwa, Mungu alikuwepo na aliumba. Kumjua Mungu zaidi tutasoma maono matatu ya Mungu yaliyonakiliwa katika Bibilia.

## Funzo la Bibilia - Maono ya Mungu – Ezekieli

Mungu hujitambulisha kulingana na mahitaji wa yule ambaye anajitambulisha kwake. Tutasoma maono ambayo Mungu alimpa Ezekieli.

## Muktadha wa Maono

Ezekieli alikuwa nabii na kuhani wa Mungu. Ezekieli pamoja na wale wawili kati ya kumi na mbili wa kabla la Israeli ya kale walikuwa matekwa katika nchi ya ugeni (Ezekieli 1:1). Walikuwa mbali na mahali pao pa ibaada, mji wa Yerusalemu. Walikuwa watu waasi waliowaabudu miungu wa nchi zingine. Basi Mungu alituma neno la picha kwa njia ya maono kwa nabii na kuhani wake Ezekieli (Ezekieli 1:3).

Soma **Ezekieli 1:15-21**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome tena kwa mara nyingine.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo matano yaliyoorodheshwa katika kifungu hiki cha Bibilia. Andika majibu katika madaftari yenu.

**Mstari wa 15** Viumbe hai

**Mistari ya 16-17** Magurudumu- kutoka sehemu moja hadi nyingine.

**Mstari wa 18** Macho

**Mstari wa 19** Ulimwengu - magurudumu yanainuliwa juu ya ulimwengu.

**Mstari wa 21** Roho

Kuepuka kupeana maana ya kifungu isiyo sawa, uliza maswali yafuatayo:

**Ni nani wahusika katika kifungu hiki?** Read **Ezekieli 1:1-3**

Ezekieli, Mungu, Watumwa (Watu kutoka kwa makabila mawili ya Israeli ya kale), Watu kutoka Chaldi.

**Ni nani anayezungumza?**

'Mimi' Ezekieli.

**Ni nani wanayezungumza naye?** Soma **Ezekieli 1:28-2:5**

Makabila mawili ya Israeli ya kale.

**Wahusika wanashirikiana kwa njia ipi?**

Mungu anajionyesha kwa maono na kisha anazungumza na Ezekieli. Ezekieli anatazama na kusikia.

**Kitendo hiki kilifanyika wapi?**

Katika nchi ya kigeni ya Wachaldea karibu na mto.

**Kitendo hiki kilitokea lini? Kabla au baada ya Yesu kuwa mwili na damu, akafa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu?**

Wakati Israeli ilipochukuliwa mateka katika nchi ya wachaldea. Kabla Yesu awe mwili na damu.

**Magurudumu yanayosonga yanawakilisha kitu gani?**

Katika tamaduni za mashariki, gurudumu lawakilisha mwendo wa maisha au mzunguko wa maisha, ambapo muda hauna mwanzo wala mwisho.

**Je, mwendo wa magurudumu wamaanisha nini kumhusu Mungu?**

Mungu yuko kila mahali. Hazuiliwi katika hekalu kule Yerusalemu au katika sehemu moja au nchi. Hana mwanzo wala mwisho.Mungu anadumu milele... Mungu aliye zaidi ya wakati na mipaka ya nafasi.

**Je, macho yanamaanisha nini kumhusu Mungu? Soma Ezekieli 8:12**

Mungu huona kila kitu, ikiwemo uasi wao, unyonge wao, tamaa zao wa kimwili, ibada zao kwa miungu wao, hata inapofanywa katika siri. Hata hivyo, Mungu angali anataka kuwaweka watu wake huru kutokana na utumwa wa aina hii.

**Kwa nini kifungu hiki kiliandikwa?** Soma **Ezekieli 11:16-25**

Mungu alimpa motisha Ezekieli kwa kujionyesha kuwa Yeye ni Mungu wa ulimwengu wote,

anayejua yote, anayeona yote na mwenye nguvu zote. Hata katika nchi ya kigeni, Mungu yuko pamoa na Ezekieli na watu. Anataka kuwaweka watu wake huru kutokana na tamaa zao za mwili na kuwaabudu miungu wengine.

**Ni mambo yapi katika kifungu ambayo yanafanana siku ya leo?**

Mungu ni yule yule jana,leo na hata milele.Yeye ni Mungu wa kila mahali, anajua mambo yote na anaona kila kitu. Anataka kuwaweka watu huru kutokana na utumwa wa miili yao na kuwaabudu miungu mingine.

**Hii yamaanisha nini kwetu siku ya leo? Jadili kama kikundi.**

Kujua kwamba Mungu ni Mungu wa kila mahali, anayejua kila kitu na anaona kila kitu yamaanisha kwamba, haijalishi tulipo, haijalishi unyonge wetu, haijalishi hali zetu, Mungu yuko nasi. Anataka kujitambulisha kwetu, kutuweka huru na kutulinda.

**Ni kitu gani kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu katika kipindi hiki?**

Mungu anapita mipaka ya wakati na anga. Yuko na watu wake bila ya kujali wako wapi na wanapitia hali gani. Mungu anajitambulisha kumhakikishia Ezekieli na watu kwamba yuko nao hata katika nchi ya kigeni.

Mungu hazuiliwi na hali. Daima ana hamu ya kuwa nasi, kuwa na uhusiano nasi, kutuona kila wakati na kutushughulikia. Pia anajua kila jambo na kila mara anamfuata kila mtu kwa upendo, hata wale wanaomkataa. Yesu aliwafilia wote akijua kwamba kutakuwepo na wale ambao kamwe hawatamfuata. Ah,upendo ulioje!

**Ni nini jibu lako/sala ya kweli?**

## Sala ya kufunga ya shukrani

Muulize mmoja wenu amrudishie Mungu shukrani kwa kuwa Anataka kujitambulisha kwetu.

# Awamu ya 3: Kujionyesha Kibinafsi

*Mungu ana uhusiano.  Mawasiliano yake ni ya kibinafsi.*

## Sala ya kufungua

**Muulize mmoja wenu afungue kikao kwa maombi.**

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni wimbo moja au mbili za ibaada zinazotangaza kwamba Mungu anataka kujitambulisha kwetu, kutufikia katika hali zetu kulingana na mahitaji yetu.

## Somo la Bibilia - Maono ya Mungu – Yakobo

Kama vile tulivyojifunza, Mungu hujitambulisha kupitia kwa njia tofauti za mawasiliano.  Mungu hujitambulisha kulingana na mahitaji ya yule ambaye anajitambulisha kwake. Tutasoma maono ya Mungu yaliyopewa Yakobo.

## Muktadha wa Maono

Yakobo, ambaye alikuja kuwa baba wa makabila kumi na mawili ya Israeli ya kale, alikuwa mwana wa Isaka na Rebeka.  Isaka alikuwa mwana wa Abrahamu na Sara.  Abrahamu na Isaka walipokea ahadi ya kibinafsi kutoka kwa Mungu.  Yakobo alikua amemdanganya ndugu  yake mkubwa ili aweze kupata baraka ya mtoto wa kwanza.  Kutokana na haya, Rebeka mama wa Yakobo alimwambia Yakobo atoroke kutokana na hasira ya ndugu yake.  Yakobo alikuwa amewadia wakati wa kuoa, basi Isaka alimtuma Yakobo aende kwa familia ya Rachel kutafuta mke. Katika safari yake alikutana na Mungu.

*Soma* **Mwanzo 28:10-22**

Tafakari kifungu hiki na ukisome tena mara kadha.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyapata katika fungu hili la Bibilia. Yaandike majibu yako katika daftari yako.

Kuepuka kupeana maana ya kifungu isiyo sawa, uliza maswali yafuatayo:

**Ni nani wahusika katika kifungu hiki?**

Mungu, Yakobo na malaika wa Mungu.

**Ni nani anayezungumza?**

Mungu.

**Wanazungumza na nani?**

Yakobo.

**Je, wahusika hawa wanashirikiana kwa njia gani?**

Mungu anajitambulisha katika maono na kisha anazungumza na Yakobo. Yakobo anatazama na kusikiza.

**Je Mungu anajifahamisha kwa Yakobo kwa njia gani? Soma mstari wa 13**

Mimi ni Bwana, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka.' (SUV)

**Je, njia ambayo Mungu anajifahamisha kwetu yatuambia nini kuhusu uhusiano wake na Yakobo?**

Yakobo hakuwa na uhusiano wa karibu na Mungu. Yakobo alimjua kumhusu Mungu wa baba yake, bali hakuwa amekumbana na Mungu yeye mwenyewe.

**Je, ni kitu gani ambacho Mungu alimwahidi Yakobo katika mstari wa 15?**

Mungu alimwahidi Yakobo kwamba, Atakuwa naye, Atamlinda popote aendapo na Atamrudisha katika nchi hii; Mungu hatamwacha.

**Mambo haya yalifanyika wapi? Soma mstari wa 19**

Katika mji uitwao Luz, kwa sasa Yakobo aliupatia mji huo jina Bethel.

**Ngazi ilikuwa imewekwa wapi na ngazi hio ilienda wapi?** Soma **mstari wa 13**

Ngazi hio ilikuwa ulimwenguni na ilienda mbinguni.

**Ngazi hiyo yawakilisha nini?**

Ngazi yamaanisha uhusiano wa Mungu na watu. Mungu anashuka chini kutoka mbinguni hadi ulimwenguni, anajileta kwetu. Mungu alimwonyesha Yakobo uhusiano wake wa kibinafsi, maono kutoka ulimwenguni ambapo aliishi, akitazama juu mbinguni, ambapo Mungu anaishi.

**Mambo haya yalifanyika lini? Kabla au baada ya Yesu kuwa mwili na damu, akafa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu?**

Kabla ya Yesu kuwa mwili na damu.

**Kwa nini kifungu hiki kiliandikwa?**

Katika hadithi ya kweli ya taifa la Israeli na uhusiano wao na Mungu, twajifunza mengi kumhusu Mungu. Mungu alimpatia Yakobo uhusiano wa kibinafsi kumhusu mwenyewe. Kumjua Mungu kama Mungu wa baba yake au wa baba wa baba yake haukutosha. Sasa Yakobo amjua Mungu kwa manufaa yake na kutokana na haya,anapokea ahadi yake ya kibinafsi.

**Ni mambo yapi katika kifungu ambayo yanafanana na nyakati za leo?**

Mungu ni yule yule jana, leo na milele. Mungu hujitambulisha mwenye kibinafsi na kulingana na mahitaji yetu. Kila mmoja sharti ajichagulie mwenyewe yule atakaye mwabudu.

**Hiyo yamaanisha nini kwetu leo?**

Yakobo alikuwa na maono ya Mungu kumfikia hapa ulimwenguni kutoka mbinguni. Mungu alikuja chini ulimwenguni kama mwanadamu kwa mfano wa mwili na damu. Mwana wa Mwanadamu, Mwana wa Mungu, Yesu Kristo (Aliyepakwa Mafuta).

Katika **Yohana 1:51** Yesu awaashiria wafuasi wake kwamba wataona mbingu ikifunguka wazi na malaika watashuka na kupanda na Mwana wa Mwanadamu (Yeye Mwenyewe).
Mbingu yafunguka kupitia kwa uzao, kifo, ufufuo na kupaa kwa Yesu Kristo. Leo, kupitia kwa Yesu Kristo, kwa Roho wake, twaweza kumjua Mungu kibinafsi. Tuna uwezo wa kumfikia Mungu moja kwa moja. Haijalishi hali zetu, Mungu anasubiri.

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu katika kipindi hiki?**

Mungu hujitambulisha kwa mtu kulingana na mahitaji yake. Yakobo alitaka kukumbana na Mungu yeye mwenyewe. Haitoshi kumjua Mungu wa baba zetu. Hata Yakobo alipofanya makosa, katika wakati wake wa upweke, Mungu alitaka kujitambulisha kwake Yakobo na kumbariki. Mungu ni Mungu wa uhusiano. Anashiriki ana kwa ana, Niwa upendo yuko tayari kubariki, ni mwaminifu milele na hutimiza ahadi zake zote.

**Ni nini jibu lako/sala ya kweli?**

## Maombi ya kufunga ya Shukrani

Muulize mmoja wenu amrudishie Mungu shukrani kwa sababu Anataka kujitambulisha kwetu.

# Awamu ya 4: Wakati ni Sasa

*Tazama yale macho yake kama moto! Wale wanaompokea wanaona upendo, mwangaza, maisha.*
Wale wanaomkataa wanaona hukumu, giza, kifo

## Maombi ya kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi

## Kuabudu

Kama kikundi, chagueni na muimbe nyimbo mbili au tatu za kuabudu ambazo zatangaza kwamba Yesu ni njia ya kuenda mbinguni.

## Somo la Bibilia - Maono ya Mungu - Yohana

Jinsi tulivyojifunza, Mungu hujidhihirisha kupitia kwa njia tofauti za mawasiliano. Mungu hujionyesha kulingana na mahitaji ya yule ambaye anajionyesha kwake. Tutajifunza kuhusu maono ambayo Yohana alipewa na Mungu.

## Muktadha wa Maono

Yohana alihamishwa kwa sababu ya Imani yake. Kanisa lilikuwa chini ya mateso. Utawala mbaya na wenye ukatili mwingi ulikuwa mamlakani—Warumi. Katika hali ya kukandamizwa na upweke, Yohana alipokea ufunuo wa Mungu katika ukuu, upendo na nguvu zake. Mungu alikuwa, yupo na atakuwa kwenye kiti cha enzi na nguvu zake ni kubwa kuliko maovu yote na utawala wa mwanadamu wa nyakati zote zikijumulishwa pamoja. Yohana na waumini wote wanaweza kuwa na hakikisho kwamba mwisho wa maovu unakuja. Yesu ameshinda maovu. Wakati wa maovu utaisha. Mungu anawasubiri wote watakaokuja kwake kwa hiari yao kabla ya maovu hayajaangamizwa.

Hebu tuangalie sehemu kidogo tu ya ufunuo wa Yesu na mambo yanayofanyika.

Soma **Ufunuo wa Yesu 4:1-11**

Tafakari kuhusu kifungu hiki na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadilieni kuhusu mambo yaliyoorodheshwa katika kifungu cha Bibilia, mstari baada ya mstari. Andikeni majibu katika daftari zenu.

**Mstari wa 1** mlango uliofunguliwa wa mbinguni.

**Mstari wa 2** Kule mbinguni, kiti cha enzi na aliyekikalia kiti hicho.

**Mstari wa 3** Upinde wa mvua umezunguka kiti cha enzi.

**Mstari wa 4** Karibu na kiti cha enzi, kuna viti vingine ishirini na nne vya enzi ambavyo vime-kaliwa na wazee ishirini na wa nne.

**Mstari wa 5** Ngurumo, radi na sauti kutoka kwa kiti cha enzi. Taa saba= roho saba za Mungu.

**Mstari wa 6** Bahari la glasi. Viumbe hai vinne vilivyojaa macho.

**Mstari wa 7** Kiumbe hai cha kwanza ni kama simba. Kiumbe hai cha pili ni kama ndama. Kiumbe hai cha tatu ni kama sura ya mwanadamu. Kiumbe hai cha nne ni kama tai anayepaa.

**Viumbe hawa wenye uhai wanne wanasema kitu gani usiku na mchana?** Soma **mstari wa 8**

*'Mtakatifu, Mtakatifu,Mtakatifu Bwana Mungu Mwenyezi, Aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja!' (SUV)*

**Ni mambo yapi ambayo wazee hao ishirini na wanne wanafanya wakati ambapo viumbe wenye uhai wanne wanapomwabudu yule aliyeketi kwenye kiti cha enzi?**

Soma **mistari ya 9-10**

Wanaanguka chini mbele ya Yule aliyeketi kwa kiti cha enzi na kumwabudu.

**Ni mambo yapi ambayo wazee hao ishirini na wanne wanasema wanapomwabudu aliyeketi kwa kiti cha enzi?**

Soma **mstari wa 11**

*'Ewe, Bwana wetu na Mungu wetu, unastahili kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa.' (SUV)*

Mlango uliofunguka kuingia mbinguni: Mlango ambao Yohana auonao waashiria mwili kamili wa Yesu na damu ya sadaka. Tunapopokea sadaka ya Yesu mwenyewe, pia tunapata Roho wa Mungu ndani yetu, uwepo wake juu yetu na unaotuzingira.

Yesu, Mungu ambaye alikuwa mwili na damu, mmoja wetu, aliyatoa maisha yake kama sadaka, akafufuka na akapaa juu na hivi sasa,ameketi kwenye mkono wa kulia wa Mungu Baba, aliyafanya hayo yote, ili kwa Roho wake, tuwe na uwezo wa kuingia katika chumba cha enzi cha Mungu.

Hii ni yetu kwa sasa, katika huu ulimwengu ulioharibiwa na maovu. Katika roho,tuna uwezo wa kuingia katika chumba cha enzi cha Mungu, kwa mkutano wa kila mara, ushirika, ushauri, uhusiano, upendo na ufunuo.

Nyakati za usoni ni tegemeo letu kwamba, tutakuwa na uwezo wa kuingia katika chumba cha enzi cha Mungu tukiwa katika miili yetu kamilifu iliyofufuka, ambapo tutamwona uso kwa uso. Hakutakuwa na machozi, machungu, kuzeeka na magonjwa. Kila kitu kitakamilishwa katika utimilifu wa wakati.

Kuepuka kupeana maana ya kifungu isiyo sawa, uliza maswali yafuatayo:

**Wahusika katika kifungu hiki ni akina nani?**

Yohana, sauti, Mungu (Yule aliyeketi kwenye kiti cha enzi), viumbe wanne, wazee ishirini na wanne, roho saba za Mungu.

**Ni nani anayezungumza?**

Yohana ambaye ni mwandishi,sauti (mstari wa 1), wale viumbe wanne (mstari wa 8) na wazee ishirini na wanne (mstari wa 11).

**Wanawaongelesha akina nani?** Soma **Ufunuo wa Yesu 1:4**

Yohana anawaongelesha Waumini wa nyakati hiyo na wa kwa nyakati zote

**Sauti inamuongelesha nani?** Soma **Ufunuo wa Yesu 4:1**

Sauti inamuongelesha Yohana.

**Viumbe hao wenye uhai wanne wanamuongelesha nani?** Soma **Ufunuo wa Yesu 4:8**

Viumbe hawa wenye uhai wanne wanazungumza kuhusu sifa ya yule aliyeketi katika kiti cha enzi (Mungu).

**Wazee hao ishirini na wanne wanamuongelesha nani?** Soma **Ufunuo wa Yesu 4:11**

Wazee ishirini na wanne wanazungumza kuhusu sifa ya yule anayeketi kwa kiti cha enzi (Mungu).

**Je, wahusika wanashirikianaje?**

Yohana akiwa katika roho anaingia mbinguni, anatazama na kusikiza sauti, viumbe hai wanne na wazee ishirini na wanne wanamwabudu Yule anayeketi katika kiti cha enzi (Mungu).

**Kioja hiki kilifanyika wapi?** Soma **Ufunuo wa Yesu 1:9** na **Ufunuo wa Yesu 4:1**

Kisiwa cha Patmos na mbinguni

**Kioja hiki kilifanyika lini? Kabla au baada ya Yesu kuwa mwili na damu, akafa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu?** Soma **Ufunuo wa Yesu 1:17- 18**

Baada ya Yesu kuwa mwili na damu,akafa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu.

**Kwa nini kifungu hiki kiliandikwa?**

Kumtambua Mungu mmoja wa kweli - mkuu, mwenye nguvu zote,wa milele, anayejua kila kitu, mtakatifu - Yule anayetawala na kutamalaki, aliumba vitu vyote, ni mwaminifu na anastahili sifa zote na kuabudiwa.

Kuwahimiza waumini wote kwa nyakati zote kwamba kupitia kwa Yesu (mlango ulio wazi) tuna uwezo wa kuingia mbinguni, kwa yule anayeketi kwa kiti cha enzi, wakati wowote au katika hali yoyote.

**Ni baadhi mambo gani katika kifungu ambayo yanafanana wakati huu?**

Mungu, mkuu, mwenye nguvu, wa milele, anayejua kila kitu, mtakatifu–Yule anayetawala na kutamalaki, aliumba vitu vyote, ni mwaminifu na anastahali sifa zote na kuabudiwa.

**Hii yamaanishi nini kwetu wakati huu?**

Wakati tunapopokea dhabihu ya Yesu iliyo katika mwili na damu yake mwenyewe, kwa kiroho twaweza kuingia uwepo wake, na kuingia kwa ujasiri kwa kiti chake cha enzi kilicho mbinguni wakati wowote. Hata katika nyakati za machungu, upweke na mateso Mungu hutawala kwa ukuu na Mungu hujileta kwetu wakati wowote.

**Ni kitu gani kingine kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu kutokana na kikao hiki?**

Mungu ni mkuu, mwenye nguvu zote, mtakatifu-Yule anayetawala na kutamalaki, muumba wa vitu vyote na anastahili sifa zote na kuabudiwa. Kimsingi, Yesu ni njia ya kuenda mbingu ni, mlango ulio wazi.

## Toa Ushuhuda

Muulize kila mmoja aseme kwa sentensi moja au mbili kuhusu kile ambacho Mungu amekuwa akiwazungumzia kupitia kwa vikao vya maono ya Mungu.

**Ni nini jibu lako/sala ya kweli?**

# Awamu ya 5: Kwa maana Mungu aliupenda

*Ufahamu ni nguvu. Kujua nguvu za upendo wake.*

## Maombi ya kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Kuabudu

Kama kikundi, chagua na muimbe nyimbo mbili au tatu za kuabudu zinazotangaza upendo wa Mungu.

## Somo la Biblia - Upendo wa Mungu

Kama tulivyojifunza kuhusu Mungu aliyekuwa, na yuko na atakuja ni Mungu wa uhusiano. Mungu hufanya kila kitu kutokana na upendo kwa sababu Mungu anapenda. Upendo huu wa Mungu unapita uwezo wetu wa kuelewa. Tutasoma mambo kadhaa ya upendo wa Mungu kutoka kwa hadithi yake, hadithi yake ya kweli ya upendo, Biblia.

Soma **Wakorintho wa kwanza 13:1-8**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara mingi

## Mjadala wa Kikundi

Jadili kuhusu maswala ya upendo wa Mungu ambayo yameorodheshwa katika kifungu hiki cha Biblia, mstari baada ya mstari.

Andika majibu katika madaftari yenu.

**Mstari wa 4** Ana subra (husubiri kwa muda mrefu bila hasira), upole, hauna wivu, majivuno na kiburi

**Mstari wa 5** Haina tabia ya ujeuri, hatafuti mambo yake binafsi, hakasirishwi na hafikifirii maovu.

**Mstari wa 6** Hafurahii mabaya, bali hufurahi pamoja na ukweli.

**Mstari wa 7** Haukati tamaa, huamini yote,hutumaini yote, hustahimili yote.

**Mstari wa 8** Upendo hauishi na hautawahi isha

Ni nani chanzo cha upendo huu? Soma **Yohana wa kwanza 4:7-10**

## Mjadala wa Kikundi

Jadili jinsi ambavyo upendo wa Mungu umeonyeshwa kwetu katika kifungu hiki cha Biblia. Andika majibu katika madaftari yenu.

Mungu anatupenda sana hadi alimtuma mwana wake kuwa dhabihu ya mwili na damu kwetu, akachukua adhabu yetu, ili tuweze kuishi kupitia kwake. Kuepuka kupeana maana ya kifungu isiyo sawa, uliza maswali yafuatayo:

**Wahusika ni nani katika kifungu hiki?** Soma **Yohana wa kwanza 4:7-10**

Yohana mwandishi, waumini(wapendwa), Yesu (Mwana wa Mungu) na Mungu.

**Ni nani anayezungumza?**

Yohana mwandishi

**Wanamuongelesha nani?**

Yohana anawaongelesha waumini wakati huo na kwa nyakati.

**Wahusika wanashirikiana kwa njia gani?**

Yohana awaandikia waumini barua.

**Kioja hiki kilifanyika lini? Kabla, au baada ya Yesu kuwa mwili na damu, akafa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu?**

Baada ya Yesu kuwa mwili na damu, akafa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu.

**Kwa nini kifungu hiki kiliandikwa?** Soma **Yohana wa kwanza 1:1-4**

Yohana mwandishi alikuwa shahidi wakati ambapo Yesu alikuwa mwili na damu, alipokufa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu. Ili kuwezesha furaha ya muumini kukamilika, Yohana anaandika na kushuhudia kwamba, katika kuamini na kupokea dhabihu ya Yesu, dhambi zao zinasamehewa na wanakuwa wasafi.

**Ni baadhi ya mambo gani katika kifungu ambayo yanafanana na wakati huu?**

Mungu, upendo wake ambao kamwe hauishi, dhabihu yake na msamaha kwa nyakati zote hapo awali, wakati huu na wakati ujao, dhambi ambazo tumezungumza, tukawaza na kutenda dhidi ya Mungu na dhidi ya kila mmoja.

**Hio yamaanisha nini kwetu wakati huu?**

Tunapoipokea dhabihu ya mwili na damu ya Yesu mwenyewe, kiroho tunakuwa wasafi na kusamehewa milele kwa nyakati iliopita, wakati uliopo na unaokuja kwa maovu yote tuliyo yasema, kuwaza na kutenda dhidi ya Mungu na dhidi ya kila mmoja. Kamwe upendo wa Mungu hauishi. Katika upendo wa Mungu, twaweza kuamini.

**Ni kitu gani kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu katika awamu hii?**

Mungu ni upendo, upendo kamili.

## Ushuhuda

Muulize kila mmoja aseme kwa sentensi mbili au tatu, kuhusu  kujua kwamba upendo wa Mungu kwao kamwe hauishi wamaanisha nini kwao?

**Ni nini jibu lako/sala ya kweli?**

# Awamu ya 6: Upendo wa Baba

*Kwa kuwa ilimpendeza Mungu kwamba ukamilifu wake wote wa kimungu uwe ndani yake na kwake yeye, kupatanisha vitu vyote na Yeye*

## Maombi ya Kufungua

Muulize mtu mmoja afungue awamu kwa maombi.

## Kuabudu

Kama kikundi, chagueni nyimbo mbili au tatu ambazo zatangaza upendo wa Mungu.

## Somo la Biblia

Mungu aliyekuwako na yuko na atakuja ana uhusiano kamili wake mwenyewe.Baba, Mwana Yesu na Roho Mtakatifu ni kitu kimoja, watu watatu ambao ni kitu kimoja. Mungu mmoja, Tutasoma kuhusu upendo wa Baba kutoka kwa hadithi yake, hadithi yake ya kweli ya upendo, Biblia. Upendo wa Baba ni mkubwa mno kwamba anampatia Mwana kila kitu.

**Soma Wakolosai 1:19-20**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili kuhusu mambo ambayo umeyaona kuhusu upendo wa Baba kutokana na kifungu hiki cha Biblia. Andikeni majibu katika daftari zenu.

Baba ana furaha sana kuwa na ukuu wote wa Mungu mwenyezi uliofunuliwa kwetu katika Yesu. Kupitia kwa Yesu kuwa dhabihu ya mwili na damu, maumbile yote yalipatanishwa kwake na amani ikarejeshwa.

**Ni baadhi ya mambo gani katika kifungu ambayo yanafanana wakati huu?**

Mungu - Upendo wake, utimilifu wake ulioonyeshwa katika dhabihu ya mwili na damu ya Yesu.

Hamna Amani bila Yesu.

**Hiyo yamaanisha nini kwetu leo?** Soma **Wakolosai 1:21-22**

Tunapopokea dhabihu Yesu ya mwili na damu, hatumpingi Mungu tena. Sasa tuko pamoja na Mungu, tumekubaliwa jinsi tulivyo na tuko katika uhusiano na Mungu, tumepelekwa kwa Mungu kama watakatifu na wasio na lawama. Hatuwezi kushtakiwa katika macho ya Mungu.

Soma **Yohana 3:16-17**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili uliyoyaona kuhusu upendo wa Baba kutoka katika kifungu hiki cha Bibilia.

Andikeni majibu yenu katika madaftari yenu.

Upendo wa Mungu ni mkubwa sana. Alitupatia kila kitu katika Yesu, ambaye alikuwa mwili na damu, akafa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu. Mungu alijitolea ili auokoe ulimwengu, na kuwa dhabihu ya mwili na damu kwa mambo yote maovu ambayo tumewahi kuyasema, kuwaza au kufanya dhidi ya Mungu au watu.

**Ni nini baadhi ya mambo katika kifungu ambayo yanafanana na wakati huu?**

Mungu na upendo wake. Maovu.

**Leo hii, hio yamaanisha nini kwetu?** Soma **Yohana 3:18**

Milele tumeokolewa kutoka kwa hukumu na adhabu. Hatutahukumiwa tena. Tuna uzima wa milele.

Soma **Yohana 3:35**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili uliyoyaona kuhusu upendo wa Baba kutoka kwa kifungu hiki cha Bibilia.

Andikeni majibu yenu katika madaftari yenu

Upendo wa Baba ni mkubwa sana kwamba anampatia Yesu, mwana wake kila kitu.

**Ni nini baadhi ya mambo katika kifungu ambayo yanafanana na ya wakati huu?**

Mungu, upendo wake na tabia yake ya ukarimu.

**Leo hii, hio yamaanisha nini kwetu?** Soma **Yohana 3:36**

Yeyote anayeamini katika Yesu, Mungu Mwana, ana uzima wa milele.

Soma **Yohana wa kwanza 3:1**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona kuhusu upendo wa Baba kutoka kwa kifungu hiki cha Bibilia.

Andikeni majibu yenu katika madftari yenu.

Mungu anatupenda sana alitupa kila kitu kupitia Yesu. Sisi ni wana wake, Yeye ni baba yetu anayetupenda kwa usawa na upendo wake kwa Mwana wake.

**Ni nini baadhi ya mambo katika kifungu hiki ambayo yanafanana na wakati huu?**

Mungu, upendo wake na wote wanaoamini na kupokea dhabihu ya Yesu ya damu na mwili ni mwana wa Mungu.

**Leo hii, hio yamaanisha nini kwetu?**

Sisi ni mwana wa Mungu, tuliokubaliwa jinsi tulivyo, tukakubaliwa katika fanilia yake, na kupokea upendo wake milele.

Soma **Wakolosai 1:12-14**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona kuhusu upendo wa Baba kutoka kwa kifungu hiki cha Biblia.

Andikeni majibu katika madaftari yenu.

Mungu anatupenda sana ametuwezesha kupitia kwa dhabihu ya mwili na damu ya Mwana wake, kupokea yote ambayo Yesu anavyo, alikuwa na atakuja. Warithi wa pamoja katika Kristo kama mwana wa Mungu.

**Ni nini baadhi ya mambo katika kifungu hiki ambayo yanafanana wakati huu?**

Mungu, upendo wake, tabia yake ya ukarimu, dhabihu ya mwili na damu ya Mwana wake.

**Hio yamaanisha nini kwetu?**

Twapokea yote ambayo Yesu anavyo, alikuwa na atakuja. Tuko huru kutoka kwa nguvu za giza.

Tu katika ufalme wa Mungu, Ufalme wake wa mwangaza, warithi wa pamoja na Yesu.

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu katika kikao hiki?**

Upendo wa Baba.

## Shuhudia

Muulize kila mmoja aseme kwa sentensi moja au mbili kuhusu anachojua upendo wa Baba wamaanisha nini kwao?

**Ni nini jibu lako au sala ya kweli?**

# Awamu ya 7: Upendo wa Mwana

*Mungu aliufanya ubinafsi wake katika upendo, ili tuweze kuwa na uhusiano naye katika upendo.*

## Maombi ya Kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni na muimbe nyimbo mbili au tatu ambazo zinatangaza dhabihu ya mwili na damu ya Yesu.

## Somo la Bibilia

Mungu ambaye alikuwa na angali, na atakuja ana uhusiano kamili na nafsi yake mwenyewe. Baba, Yesu Mwana na Roho Mtakatifu wako katika umoja uliokamilika, watu watatu kwa mmoja. Mungu mmoja. Tutasoma kuhusu uhusiano wa upendo wa Mwana wa Mungu, Yesu.

Upendo wa Yesu ni mwingi sana, aliacha kila kitu ili awe dhabihu yetu ya mwili na damu. Hata hivyo, kuujua kibinafsi upendo wake zaidi na zaidi kila siku yatusaidia kupokea ukamilifu wa maisha, ukweli na nguvu zitokazo kwa Mungu na ni Mungu.

Soma **Yohana 10:14-18**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona kuhusu upendo wa Yesu katika kifungu hiki cha Bibilia. Andika majibu katika madaftari yenu.

Upendo wa Yesu ni mwingi sana.  Ana uwezo wa kuyatoa maisha yake au la, lakini aliamua kuyatoa maisha yake mwenyewe ambayo ni mapenzi ya Baba. Kwa maana Mungu alipenda, alitupa kila kitu kwake mwenyewe.  Yesu aliacha kila kitu na akaamua  kuwa mwili na damu, akafa msalabani, akafufuka kutoka kwa wafu na akapaa juu.  Mungu alijitoa mwenyewe kuuokoa ulimwengu, kuwa dhabihu ya mwili na damu ya milele kwa makosa yote ambayo tumewahi kusema, kuwaza au kufanya dhidi ya Mungu au wanadamu.  Yesu anaendelea kujitoa mwenyewe, maisha yake ya ufufuo, upendo, ukweli na nguvu na mamlaka juu ya pepo wabaya na mwili wetu kila siku.  Yeye ni mchungaji wetu mwema.

## Shuhudia

Muulize kila mmoja aseme katika sentensi mbili au tatu, kujua kwamba Yesu ni mchungaji wao mzuri yamaanisha nini kwao?

Soma **Zaburi 23**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadha.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili kile ambacho Yesu mchungaji mwema anakufanyia. Andika majibu katika madaftari yako.

Daima Yesu ananipa kila kitu ninachohitaji.

Yesu hunipumzisha na kunipa chakula.

Yesu huniburudisha na kunipa maji ya uzima.

Yesu hurejesha roho yangu, akili na mwili.

Yesu huniongoza katika kujua utakatifu wake na haki, kwa heshima yake.

Hata nikitembea katika bonde la kivuli mauti, sina hofu kwa kuwa Yesu yuko nami.

Yesu hunituliza kwa upendo wake, uhusiano wake nami na nguvu zake kuu na mamlaka.

Yesu ananitayarishia karamu mbele ya adui wangu ili waone. Yesu ananifanya niwe mgeni wake wa heshima.

Yesu ananipaka mafuta yake kwa wingi wake usio na mwisho na uzuri wote wa Mungu.

Bila shaka, rehema ya Mungu yanifuata maisha yangu yote, kwa sasa kama mwili na damu. Milele na milele nitaishi na Mungu.

**Ni nini baadhi ya mambo katika kifungu hiki ambayo yanafanana wakati huu?**

Yesu ni mchungaji mzuri ambaye anaendelea kujitoa kwa kondoo wake.

**Hio yaamanisha nini kwetu leo?**

Twaweza kutulia katika Yesu, jinsi ilivyo, aliyofanya, anayofanya na alivyoahidi Atafanya .

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kuhusu Mungu katika kikao hiki?**

Mungu katika Yesu anajitolea kwetu kabisa kwa sababu anapenda.

**Je upendo huu wa Mungu katika Yesu una nguvu kiasi gani?** Soma **Warumi 8:38-39**

Upendo wa Mungu kwetu katika Yesu ni mkubwa na wenye nguvu Zaidi kuliko chochote, hata pamoja na unyonge wetu na uovu wa huu ulimwengu.

**Ni nini jibu lako /sala ya kweli?**

# Awamu ya 8: Upendo wa Roho Mtakatifu

*Roho na Bi Harusi wanasema 'Njooni!' Wacheni wote wanaosikia waseme njoo.*
*Njooni nyinyi nyote wenye kiu. Wacha wote wanaotamani maji ya uzima wachukue bure.*

## Maombi ya Kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni wimbo moja au mbili zinazotangaza upendo wa Mungu.

## Somo la Bibilia

Mungu aliyekuwepo, aliye kwa sasa na atakayekuja ana uhusiano kamili naye mwenyewe. Baba, Yesu Mwana na Roho Mtakatifu wamo katika umoja kamili, watu watatu katika mmoja. Mungu mmoja. Tutasoma uhusiano wa upendo wa Roho Mtakatifu.

Upendo wa Mungu ni mkubwa sana, unapita uwezo wetu wa kuelewa. Upendo wa Roho Mtakatifu haujielekezi kwake binafsi. Badala yake, unatambua, unathibitisha, unabadilisha na kukaa ndani yetu, ili tuweze kuhisi upendo wa Baba na upendo wa Yesu Mwana, kibinafsi, kwa nguvu kuu na kwa ukaribu.

**Roho Mtakatifu anashuhudia kumhusu nani na kuleta utukufu kwake?** Soma **Yohana 16:13-15**

Yesu.

**Je, upendo wa Mungu unamwagwa kwa njia gani ndani ya mioyo yetu, kibinafsi, kwa nguvu kuu na kwa ukaribu?**

Soma **Warumi 5:5-8**

Kwa Roho Mtakatifu ambaye tumepewa wakati tunapoipokea zawadi ya bure ya Yesu anapojitoa mwenyewe

Soma **Warumi 8:14-16**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyagundua kuhusu upendo wa Roho Mtakatifu kutoka kwa kifungu hiki cha Bibilia. Andika majibu katika madaftari yenu.

Upendo wa Mungu ni mwingi kwamba, muda tu tunapoipokea zawadi ya Yesu ya kujitoa mwenyewe, tunapokea Roho wa Yesu, Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu ndani yetu. Sisi ni wana wa Mungu na Mungu ni Baba yetu wa upendo.

Waumini wote (waume kwa wake) ni 'wana wa Mungu' kwa sababu wanapokea Roho wake.

Maneno ‘wana wa Mungu’ yaonyesha aina ya uhusiano na Mungu ambao sasa tunarithi. Kupitishwa huku ni kama wa mwana wa kwanza wa damu ya kifalme, na haki zote za kisheria na mwana wa kwanza wa kiume. Kwa hivyo, tunakuwa warithi sawa na Yesu, Mfalme wa Ufalme wa Mungu.

## Shuhudia

Muulize kila mmoja aseme kwa sentensi moja au mbili, kujua kwamba wao ni wana wa Mungu (mwana wa kwanza wa ukoo wa kifalme) yamaanisha nini kwao?

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu kutokana na kikao hiki?**

Mungu katika Yesu amejitolea kwetu kikamilifu, anatupa Roho wake wa kufanywa kuwa wana, kwa sababu Mungu alipenda.

**Ni nini jibu lako/sala ya kweli?**

# Awamu ya  9: Kukubaliwa jinsi nilivyo

*Kupatikana katika upendo wake.  Kukubaliwa jinsi nilivyo.  Nimefungwa milele.  Katika utimilifu wa maisha.  Nimebadilishwa milele.  Na Yule Mkuu.*

## Maombi ya Kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni na muimbe nyimbo mbili au tatu zinazotangaza kwamba nakubaliwa na Mungu jinsi nilivyo.

## Warsha ya Kadi Nne

**Hatua ya  1:** Kila mmoja achukue karatasi na aikate kwa vipande vinne.  Kila mmoja achore mbele ya hio karatasi picha inayowakilisha kila kitu kilichoorodheshwa hapa chini.



Kadi 1 = Mimi mwenyewe.  Kadi ya  2 = Familia yangu.  Kadi ya 3 = Masomo yangu.

Kadi ya  4 = Kijiji changu.

**Hatua ya  2:** Kila mtu aeleze jinsi alivyo, familia yao, shule yao na jamii yao kupitia kwa michoro sanifu na maneno nyuma ya kila mojawapo ya hizo kadi nne.  Majina yasiandikwe kwenye kadi hizo.

Kadi ya  1: Nahisi namna gani kuhusu jinsi nilivyo? (Chora sura ya furaha au huzuni). Nahisi napendwa? Nahisi nakubaliwa na jamii yangu? Mimi ni mzuri kwa jambo gani? Napenda kufanya nini? Nampenda mnyama yupi? Napenda chakula kipi? Ndoto zangu ni gani? Nahofia kitu gani?

Kadi ya 2: Nani aliye katika familia yangu? Hali ya afya ya familia yangu iko namna  gani? Ni mungu yupi au mgani anayeaminiwa na familia yangu? Walio juu yangu kimamlaka ni watu wa aina gani? ( Chora sura ya furaha au huzuni).

Kadi ya 3: Nahisi namna gani kuyahusu maisha yangu? (Chora sura ya furaha au ya huzuni). Ni kitu kipi kimoja ambacho nilijifunza nilipokuwa mtoto?  Mtu aliyenifunza mambo haya alikuwa wa aina gani?  Nilipenda somo lipi au kujifunza jambo gani?  Somo lipi lilikuwa gumu au jambo lipi lilikuwa gumu kujifunza?  Somo lipi lilikuwa rahisi kuelewa au jambo lipi lilikuwa rahisi kujifunza?  Sehemu ambazo sihisi usalama ziko wapi?   Sehemu ninazohisi ni salama ziko wapi?

Kadi ya 4: Ni kitu gani ninachokipenda kuhusu mahali ninapoishi? Ni kitu gani ambacho sipendi kuhusu mahali ninapoishi? Wazee wanaoishi mahali ninapoishi wanafanya nini? Je wazee hawa wananisaidia kwa njia gani?

**Hatua ya 3:** Baada ya kila mtu kumaliza kujaza mambo katika kadi zao, wanapaswa kukupa kadi hizo. Kadi hizo ziwekwe katika mpangilio wa kadi nne.

**Hatua ya 4:** Mpatie kila mmoja kadi nne ambazo sio zake. Hamna anayepaswa kumjua mwenzake na wala asijue kadi zake zimepatiwa nani.

**Hatua ya 5:** Moja kwa moja, kila mmoja aambie kikundi kuhusu kadi nne ambazo amepatiwa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili matokeo ya kila kifurushi cha kadi.

**Kuna mpangilio au uhusiano upi kati ya jinsi ambavyo kila mtu anahisi kujihusu mwenyewe na hali zao?**

**Kuna mambo gani tofauti kati ya kila mtu?**

Sote twataka tukubaliwe. Sote twataka tupendwe. Tunapotafuta kukubaliwa au kupendwa na wengine, wao na hali hii wana uwezo wa kututhibiti.

Soma **Mwanzo 29:31-35**

## Mjadala wa Kikundi

Jadili kuhusu mambo mliyoyaona kumhusu Leah na Mungu. Andika majibu katika daftari zenu.

**Mstari wa 31** Mungu alijua nini kumhusu Leah?

Hakupendwa.

**Mstari wa 32** Leah alikuwa anatumai kitu gani kingefanyika baada yake kujifungua mwana wa kiume?

Mume wake angempenda.

**Mstari wa 33** Je, mume wa Leah alimpenda baada yake kujifungua mwana wa kiume?

La.

**Mstari wa 34** Baada ya Leah kujifungua watoto watatu wa kiume, je mumewe alimpenda?

La.

**Mstari wa 35** Baada ya kujifungua watoto wanne wa kiume, Leah alisema nini?

Sasa nitamsifu Bwana.

Mungu huona azma yetu ya kutaka kupendwa, kukubaliwa. Mungu alimpa Leah tamaa ya moyo wake ya kuwa na mwana wa kiume ili amwonyeshe jinsi anavyompenda. Mungu pia alikuwa na nafasi ya Leah katika mpango wake. Kupitia kwa mwanawe wa nne wa kiume ndipo kabila ambalo Yesu, Mungu aliyekuja kuwa mwili na damu alizaliwa. Mojawapo ya makabila kumi na mawili ya Israeli. Tunapojua jinsi ambavyo Mungu anatupenda, jinsi anavyotukubali kama tulivyo, jinsi tunavyopendeza machoni pake, na kwamba alituchagua kabla ya kuumba ulimwengu ili tuwe sehemu ya mpango wake, ndipo tunapowekwa huru wa kutotaka kupata upendo au idhini ya watu wengine. Twaishi katika ukweli kwamba upendo wake na idhini yake imetosha zaidi.

**Tumepewa mamlaka ya kufanya nini tunapojua kwamba tunakubaliwa jinsi tulivyo?** Soma **Warumi 15:7**

Tumepewa mamlaka ya kuwakubali wengine jinsi walivyo kama vile mimi nimekubaliwa jinsi nilivyo.

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kuhusu Mungu kutokana na kikao hiki?** Soma Matendo ya **Mitume 10:34**

Mungu huwakubali watu wote jinsi walivyo. Amenikubali mimi jinsi nilivyo.

**Ni nini jibu lako/sala ya kweli?**

# Awamu ya 10: Kitambulisho-Kuzaliwa kwa Roho

*Mungu: Roho aliyezaliwa kwa mwili na damu, ili awe dhabihu ya mwili na damu kwa wote wanaozaliwa kwa mwili na damu ili wao kama mwili na damu waweze kuzaliwa kwa Roho.*

## Maombi ya Kufungua

Muulize mmoja wenu afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi chagueni na muimbe nyimbo mbili au tatu za ibaada ambazo zitangaza kwamba nimezaliwa na Roho, mtoto wa Mungu.

## Somo la Bibilia

Kama vile tulivyojifunza, waumini wote wanaopokea  dhabihu ya mwili na damu ya Yesu mwenyewe hupokea Roho wa Mungu–Roho Mtakatifu wa undani.  Huu ni wakati wetu wa kurithi sisi ni Watoto wa Mungu.

(kama mwana wa kwanza wa kiume wa damu ya kifalme), warithi wa pamoja na Yesu, kuishi katika ufalme wa Mungu hapa ulimwenguni katika dunia iliyoharibiwa na uovu.

Mungu alichagua kuwa mmoja wetu kwa sababu  anatupenda na katika wakati huo wa historia, Yesu, kupitia kwa mbegu ya Roho Mtakatifu, alizaliwa kwa mwanamke kama mwili na damu, ili sisi tuliozaliwa katika mwili na damu, kupitia kwa kuamini na kupokea dhabihu ya milele ya mwili na damu ya Yesu, tunazaliwa katika Roho.

Soma **Yohana 1:12-13**

Tutajifunza ni kwa nini mwanadamu aliyezaliwa katika mwili na damu alipaswa kuzaliwa kwa Roho katika hadithi ya Mungu, hadithi yake ya upendo wa kweli, Bibilia.

Soma **Wakorintho wa Kwanza 15:47-51**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona kumhusu mwanadamu wa kwanza (aliyezaliwa katika mwili na damu) na mwanadamu wa pili (Yesu wa Roho aliyefanywa kuzaliwa kwa damu na mwili) kutoka katika kifungu hiki cha Bibilia.

Andika majibu katika madaftari yenu.

**Mwanadamu wa kwanza aliumbwa kutoka kwa kitu gani?**

Mchanga

**Ni mfano wa nani na kutambulishwa ambao tunao kabla ya kupokea dhabihu ya Yesu ya mwili na damu yake mwenyewe?**

Mwanadamu wa kwanza - mwanadamu wa mchanga.

**Ni mfano wa nani na kutambulishwa ambao tunao kabla ya kupokea dhabihu ya Yesu ya mwili na damu yake mwenyewe?**

Mwanadamu wa pili-Bwana kutoka mbinguni-Yesu.

Huu ni urithi wetu wa sasa. Tuna kitambulisho cha Yesu, mwili na damu iliyozaliwa katika Roho yake–Roho Mtakatifu, mwana wa Mungu (kama mwana wa kwanza wa kiume wa damu ya ufalme), warithi wa pamoja na Yesu.

kuishi katika ufalme wa Mungu hapa ulimwenguni, katika dunia hii iliyoharibiwa na uovu.

Soma **Wakorintho wa Kwanza 15:50-55**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadha wa kadha.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona kuhusu kutambulishwa kwa mwanadamu aliyeumbwa kutoka kwa mchanga (alizaliwa kwa mwili na damu) na Yesu wa Roho (aliyefanywa kuwa mwili na damu) kutoka kwa kifungu hiki cha Bibilia. Yaandike majibu katika daftari zenu

**Ni nini asili ya kitambulisho cha mwanadamu aliyezaliwa kwa mwili na damu?**

Ameharibika, hana ukweli na anaangamia na amepangiwa kufa.

**Je ni nini asili na kitambulisho cha Yesu?**

Kamwe hajaharibiwa, ni mwaminifu, anadumu milele na amepangiwa kuwa wa maisha.

Mwanadamu wa kwanza alikuwa mbegu ambayo iliharibiwa kwa kuchagua kushiriki na kuwa kitu kimoja na uongo wa Yule muovu na ufahamu wa maovu na mazuri. Kutokana na haya, watu wote wamezaliwa katika asilia hii ambayo imeharibika. Mwanadamu wa pili Yesu, kupitia kwa mbegu ya Roho Mtakatifu, mbegu ambayo kamwe haijaharibika, alizaliwa kwa mwanamke kama mwili na damu. Yesu ni dhabihu kamili ya mwili na damu.

Soma **Warumi 5:14-19**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona kuhusu matokeo ya mwanadamu aliyeumbwa kutoka kwa mchanga (aliyezaliwa kwa mwili na damu) na matokeo ya Yesu wa Roho (aliyekuwa mwili na damu) kutoka kwa kifungu hiki cha Bibilia.

Andika majibu katika daftari zenu.

**Ni nini matokeo ya makosa ya kwanza ya mwanadamu?**

**Mstari wa 16** alihukumiwa makosa

**Mstari wa 17** kifo kilitawala.

**Ni Nini matokeo ya kipawa cha bure cha mwanadamu aliyejitolea kwa wote wanaompokea?**

**Mstari wa 16** Huru kutokana na makosa, kutangazwa kwamba hatuna makosa.

**Mstari wa 17** Maisha yanatawaliwa katika Yesu.

Soma **Wakolosai 2:13-15**

**Ni nini matokeo ya makosa ya kwanza ya mwanadamu?**

**Mstari wa 13** Kifo kutokana na makosa dhidi ya Mungu na mwanadamu mwenzake na kunaswa katika tamaa mbaya za kimwili.

**Ni nini matokeo ya kipawa cha bure cha kujitolea cha mwanadamu wa pili kwa wote wanaompokea?**

**Mstari wa 13** Twapewa uzima naye jinsi tunavyosamehewa makosa yote.

**Mstari wa 14** Hatuna makosa tena.

**Mstari wa 15** Ushindi dhidi ya nguvu na mamlaka yote, ambazo zimeshindwa na sasa hazina nguvu kabisa.

Huu ni wakati wetu wa urithi. Tumesamehewa, tuko huru kutoka kwa adhabu, kifo, hukumu na makosa. Tumefanywa kuwa hai tena na tutawala miili yetu katika maisha haya, mapepo yote mabaya na nguvu zote zinazosimama dhidi ya utawala wa Yesu. Shetani na mapepo yote mabaya hawezi kutushtaki na makosa yoyote au aibu, kwa kuwa ushindi wa Yesu msalabani umemaliza nguvu zao. Sisi ni damu na mwili uliozaliwa na Roho, tukafanywa hai katika ushindi wa Yesu msalabani katika ulimwengu huu ulioharibiwa na maovu.

Pia tuna urithi wa siku za usoni.

Soma **Wakorintho wa kwanza 15:20-23**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadha.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona kuhusu matokeo ya mwanadamu aliyeumbwa kwa mchanga (aliyezaliwa katika mwili na damu) na matokeo ya Yesu wa Roho (aliyekuwa mwili na damu) kutoka kwa kifungu hiki cha Bibilia.

Andika majibu katika daftari zenu.

**Ni nani aliyefufuka kutoka kwa wafu?**

Yesu

**Ni nani watakaofufushwa kutoka kwa wafu wakiwa na miili kamili ambayo kamwe haitazeeka, kugonjeka, au kuisha wakati ambapo Yesu atakaporudi katika ulimwengu huu kwa utukufu wake wote?**

Wote ambao wanaamini na kupokea kipawa cha bure cha Yesu, mwili wake na dhabihu yake ya damu, kwa kuwa wao ni mwana wa Mungu, aliyezaliwa katika Roho.

Soma **Ufunuo wa Yohana 1:18**

**Ni nani wa Roho aliyekuwa dhabihu kamili ya mwili na roho, alikufa,akawa hai katika mwili kamili uliofufuka, akapaa mbinguni, yu hai milele na ana mamlaka juu ya kifo na uzima?**

Yesu.

Soma **Ufunuo wa Yohana 1:5-6**

**Ni nani aliye shahidi mwaminifu, mwili wa kwanza kufufuka, mamlaka ya juu na mtawala wa mambo yote?**

Yesu.

**Kwa nini Yesu alitufanyia haya yote?**
Kwa sababu anatupenda.
Tunapoamini na kupokea kipawa cha bure cha Yesu mwenyewe,dhabihu yake ya mwili na damu, na kuongeza hali ya kuwa mwana wa Mungu aliyezaliwa kwa Roho, tunakuwa kitu gani? Wafalme (watawala juu ya Shetani, mapepo waovu na juu ya mwili wetu) na makuhani

(uhusiano wa upendo na Mungu na wengine).
Ufufuo wa Yesu ndio uliokuwa ufufuo wa kwanza wa mwili kufuka, ili tusiweze tu kuishi kwa ushindi katika huu ulimwengu ulioharibiwa na maovu, lakini tuishi katika tumaini ya siku zijazo ya hali yetu ya milele - miili kamili iliyofufuka ambayo kamwe haitazeeka, kamwe haitasha kamwe haitakufa - katika ulimwengu mpya ambao hauna maovu. Wakati Yesu atakaporudi ulimwenguni, sisi ambao tumepokea kipawa cha bure cha dhabihu yake ya mwili na roho, tutarithi miili yetu kamili iliyofufuka.

Kutokana na makosa ya mwanadamu,maumbile ya Mungu yaliharibiwa. Hali ya kutokuwa na usawa, mateso, maovu na kifo yalitawala. Kwa kuwa Mungu anatawala, Yesu aliamua kuwa mwili na damu, kupitia kwa mbegu ya Roho Mtakatifu, aliyezaliwa na mwanamke. Alikuja kwa maumbile yake mwenyewe, yeye kama mwana wa kwanza wa urithi, ili sote tuwe wana, waliozaliwa kwa Roho na damu, kupokea urithi wetu wote, kwa wakati huu na siku za usoni. Halleluya!

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu kutoka kwa kikao hiki?**

Mungu anapenda na maisha ya Yesu kama damu na mwili, kifo na ufufuo ni ushuhuda na dhibitisho ya Mungu.

**Ni nini jibu lako au sala ya kweli?**

# Awamu ya 11: Kukubalika kwa Wapendwa

*Mahitaji mawili ya mwanadamu: kutaka kukubaliwa na kutaka kupendwa. Mungu alituumba tukiwa tumekubaliwa (na heshima maalum) katika yule Aliyependwa (katika Yesu aliyependwa sana).*

## Maombi ya kufungua

Muuliza mtu mmoja afungue kikao kwa maombi

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni na muimbe nyimbo mbili au tatu zinazotangaza kwamba napendwa na Mungu, nimepewa heshima maalum na baraka katika Kristo.

## Somo la Bibilia

Kama vile tuilivyojifunza, waumini wote wanaopokea dhabihu ya mwili na damu ya Yesu mwenyewe hupokea Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu aliye ndani. Huu ni wakati wetu wa kurithi. Sisi ni mwana wa Mungu (mwana wa kwanza wa kiume wa damu ya kifalme), warithi wa pamoja na Yesu, wanaoishi pamoja katika  Ufalme wa Mungu hapa ulimwenguni, katika dunia iliyoharibiwa na maovu.

Mungu alichagua kuwa mmoja wetu kwa sababu alitupenda, na katika wakati huo wa kihistoria, Yesu kupitia kwa mbegu ya Roho Mtakatifu alizaliwa kwa mwanamke kama mwili na damu, ili sisi tunaozaliwa kwa mwili na damu, kupitia kwa kuamini na kupokea dhabihu kamili ya milele ya mwili na damu ya Yesu mwenyewe twazaliwa kwa Roho.

Tutasoma kuhusu upendo wa Baba, baraka zake, mapenzi yake(matakwa ya moyo)  na lengo la wokovu la milele

kutoka kwa hadithi yake, hadithi ya upendo wake wa kweli, Bibilia.

Soma **Waifeso 1:3-14**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha  Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona.  Andika majibu katika daftari zenu.

**Ni nini mapenzi ya Mungu na mpango ambao ametufunilia sisi?** Soma **mistari ya  9-10**

Katika utimilifu wa wakati, mambo yote yanakuwa pamoja katika Kristo, zote mbili ambazo ziko katika maswala ya mbinguni na yale ya ulimwengu.

**Ni kitu gani ambacho Mungu  Baba ametupatia (wakati uliopita), basi ambacho kwa wakati huu twamiliki**? Soma **mstari wa  3**

Kila baraka ya kiroho.

**Baraka hii iko wapi?**

Katika sehemu za mbinguni.

**Sisi tuko ndani ya nani au na nani ili tupokee hili?**

Kristo Yesu.

Kwa wakati sasa, kama vile Kristo ameketi katika mahali pa mamlaka kwenye sehemu za mbinguni, basi ni hivyo na sisi.

Kwa wakati sasa,kama vile Kristo alivyotupa kila baraka ya kiroho. Mistari ifuatayo yaelezea baadhi ya maswala ya baraka hizi.

**Sisi tulio ndani ya Kristo(wakati wa sasa), tuliopatiwa na Mungu Baba (wakati uliopita)?**
Ifanye iwe ya kibinafsi na uandike Mimi kabla ya jibu lako. Soma **mistari ya 4-6**

Mfano: Nimechaguliwa kwa upendo, utakatifu, bila ya lawama na nimepitishwa kama mwana wa kiume, aliyekubaliwa (jinsi nilivyo)

katika wanaopendwa (anayependwa sana), katika mapenzi ya Baba yangu kwa kuwa hii ni matakwa ya moyo wake .

Yesu ni mwana wa Mungu 'anayependwa', kifaa kikuu cha upendo wa Baba. Sisi pia 'wana wa kiume' wa upendo wake, tuliokubaliwa (jinsi tulivyo). Twaishi kwa wakati wa sasa, ukweli wa kiroho wa uhusiano kamili wa upendo kati ya Baba na Mwana. Sisi ni matakwa ya moyo wake.

**Sisi ni nani katika Kristo (wakati wa sasa), tuliopewa na Mungu Baba (wakati uliopita)?**

Ifanye iwe ya kibinafsi na uandika Mimi kabla ya jibu lako. Soma **mistari ya 7-8**

Mfano: Nimekombolewa na kusamehewa milele na dhabihu ya mwili na damu ya Yesu mwenyewe na neema ya Mungu ambayo kamwe haiwezi kuisha na iko kwa wingi zaidi.

**Sisi ni nani katika Kristo (wakati wa sasa), tuliopewa na Mungu Baba (wakati uliopita)?**

Ifanye iwe ya kibinafsi na uandike Mimi kabla ya jibu lako. Soma **mistari ya 11-12**

Mfano: Nimeshika urithi wangu (wakati wa sasa) kwa kuwa hii ilikuwa hatma niliyopewa na Mungu na matakwa ya moyo wake, kwa sifa ya utukufu wake.

**Sisi ni nani katika Kristo (wakati wa sasa), tuliopewa na Mungu Baba (wakati uliopita)?**

Ifanye iwe ya kibinafsi na uandika Mimi kabla ya jibu lako. Soma **mistari ya 13-14**

Mfano: Nimewekwa muhuri na Roho Mtakatifu, na nina uhakika wa kutimizwa kwa urithi wangu (wakati wa sasa na unaokuja).

Kumbuka kwamba kwa wakati sasa, kama vile Kristo ameketi kwa sehemu ya mamlaka katika sehemu za mbinguni, sisi tuko vivyo hivyo. Kwa wakati sasa, kama vile Kristo alivyo, tuna kila baraka ya kiroho.

Soma **Waefeso 1:21-23**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona.  Andika majibu katika daftari zenu.

**Ni nguvu na mamlaka kiasi gani ambazo Yesu anazo wakati huu na siku zijazo?**

Soma **mstari 21**

Zaidi ya nguvu, mamlaka, uwezo, utawala na kila kitu kilichotajwa.

**Ni nani utimilifu wa Yesu?** Soma **mstari 23**

Waumini wote waliopokea dhabihu ya Yesu ya mwili na damu yake mwenyewe.

**Ni nani utimilifu wa waumini wote waliopokea dhabihu ya mwili na damu ya Yesu mwenyewe?**

Kristo Yesu

Soma **Waifeso 2:4-9**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona.  Andika majbu kwa daftari zenu.

**Tuna kitu gani katika Kristo Yesu kwa wakati huu?** Soma **mistari ya 5-6**

Ametufanya kuwa hai pamoja na Kristo.  Ametufufua ili tuketi pamoja katika sehemu za mbinguni, kwa nguvu za Kristo na mamlaka dhidi ya tamaa zetu za kimwili na Shetani na pepo zote za maovu.

**Kwa nini Mungu alitufanya tuwe na uzima na akatufufua kuketi pamoja katika sehemu za mbinguni kwa nguvu na mamlaka ya Kristo?** Soma **mistari ya 4-8**

Kwa sababu ya upendo mkuu wa Mungu kwetu sisi.  Kupitia kwa haya yote, twaweza kutambua upendo wake usio na kikomo, ukarimu, wingi wa neema na utajiri wa baraka kwetu sisi.

**Kwa nini wokovu ni kipawa kutoka kwa Mungu?** Soma **mistari ya 8-9**

Anatulinda kutokana na uovu wa kiburi chetu cha mwili kwa kipawa cha dhabihu ya mwili na damu yake mwenyewe.  Ili mtu yeyote asiwe na majivuno.

Soma **Waefeso 1:15-20**

**Ni kitu gani ambacho Mtume Paulo awaombea watakatifu?**

**Mstari wa 17** Kwamba Mungu atawapa Roho wa hekima ili waweze kumjua vizuri zaidi.

**Mstari wa 18** Kwamba Mungu atafungua akili zao ili waweze kuuona ukweli wake Zaidi, kujua

tumaini na baraka (wakati wa sasa na siku zijazo) kwa wote wanaoamini na kupokea dhabihu yake na mwili na damu yake mwenyewe, ambao ni urithi wake wa utukufu.

**Mstari wa 19** Kujua ukuu wa nguvu zake.

**Ni kitu gani kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu kutokana na kipindi hiki?**

Upendo wa Mungu, nguvu na wingi wa baraka kamwe hauishi. Ananiona kama sifa yake na utukufu.

**Ni nini jibu lako au sala ya kweli?**

# Awamu ya 12: Mahusiano

*Mjumbe wa Kongamano: ‘ Nimejifunza kuhusu uhusiano wa mzabibu, kupokea kutoka kwa Yesu, na kujisalimisha kwa mapenzi ya Baba, hii ni muhimu sana kwangu.’*

## Maombi ya Ufunguzi

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni na muimbe nyimbo mbili au tatu zinazotangaza umoja katika Yesu au uhusiano wa mzabibu na matawi na Yesu au kuishi katika upendo wa Yesu.

## Hadithi

FIKIRIA kwamba wewe ni tawi la mzabibu mkubwa.

Umeunganishwa kwa shina kuu la mzabibu, na umeachwa kwa mapenzi ya mwenye shamba.

Kile ambacho unafanya ni kuwa hapo tu, hamna lingine, kujishikilia tu kwa shina kuu.

Na kwa sababu unajishikilia kwa shina kuu, uzuri wote wa mzabibu unatoka kwa mizizi, kupitia kwa shina kuu hadi kwako. Maji yake, virutubisho vyake; kila kitu kutoka kwa mzabibu unaingia ndani yako.

Kile tu ambacho unafanya ni kujishikilia kwa mzabibu, ukipokea uzuri wake.

Siku moja, unahisi hisia ya ‘kuumwa’. Unagundua kwamba umekua.

Rundo ndogo za tunza zaanza kumea. Pop (upendo), pop, pop (furaha,amani), pop, pop, pop (uvumilivu, upole, uzuri), pop, pop, pop ( uaminifu, upole, kujithibiti).

Huku jua linapokuchoma na mvua ikikunyeshea, ndani kuna mtiririko nyororo wa maji ya uhai na virutubishi kutoka kwa mzabibu. Haya yanafanyika kwa njia gani? Haujakuwa ukifanya jambo lolote!

Kile ambacho umekuwa ukifanya ni kujishikilia kwa mzabibu, ukipokea uzuri wake.

Hayo ni mapenzi ya mwenye shamba.

## Mzabibu

Katika hali ya kiasili, maji hutiririka kutoka sehemu ya juu hadi chini, kutoka mbinguni hadi duniani yakitiririka hadi sehemu za chini. Mzabibu wahitaji maji kuishi. Bila ya maji, utakufa. Ili tawi lipokee maji, sharti linywe kutoka kwa shina kuu-pokea kutoka kwa shina kuu. Kuishi na kuzaa tunda, sharti tawi linywe maji.

*Kama ilivyo katika maswala ya kiasili, basi yako hivyo katika maswala ya kiroho kwa vile Mungu aliumba vitu vyote.*

Katika maswala ya kiroho, Maji ya Uhai hutiririka kutoka juu hadi chini, kutoka kwa kiti cha enzi cha Mungu kupitia kwa Yesu hadi kwa matawi. Matawi hayanywi kutoka kwa mvua-inaenda ndani ya mchanga na matawi kwa hakika yanakunywa kutoka kwa shina kuu, yakipokea uzuri wote wa mzabibu kutoka kwa mzizi na shina kuu.

Soma **Yohana 15:1-8**

Tafakari kuhusu kifungu hiki cha Bibilia na ukisome mara kadhaa.

## Mjadala wa Kikundi



Jadili mambo uliyoyaona.

Andika majibu katika daftari zenu.

**Mwenye bustani ni nani?**

Mungu Baba

**Ni nani aliye shina kuu la mzabibu?**

Yesu

**Ni nani aliye tawi la shina kuu la mzabibu?**

Mimi

**Kuishi yamaanisha nini?**

Yesu asema kuishi ndani yake.  Kuishi yamaanisha

kuwa mahali (mahali Fulani, nchi, uhusiano au tarajio):

endelea, kuishi, kuvumilia, kuwa mahali, kubakia au kusimama.

**Nawezaje kuishi?**

Andika jibu lako katika daftari yako.

Katika hali ya kiasili, kuishi na kuzaa tunda, sharti tawi likule virutubishi au chakula.

Soma **Yohana 4:27-38**

## Muktadha

Katika maandiko haya, Yesu anazungumza na mwanamke aliyefukuzwa kwao.  Yesu alizaliwa katika mojawapo ya makabila kumi na mawili ya Israeli ya kale. Wakati huo,mtu kutoka Israeli ya kale hakuwa akizungumza na mtu kutoka Samaria haswa mwanamke ambaye alikuwa amefukuzwa kutoka kwa watu wake. Lakini Yesu (katika hali ya kimwili na damu) alimwendea mwanamke huyu aliyefukuzwa kwao, akamzungumzia kuhusu Maji ya Uhai  (Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu) na anajitambulisha kwake yeye ni nani, chanzo cha haya maji ya uhai.

Wakati wanafunzi wa Yesu wanaporudi Yesu anawafunza kuhusu chakula chake ni kipi na kuhusu shamba la mavuno.

Kati ya kumfikia mwanamke aliyefukuzwa kwao, kujitambulisha yeye ni nani na kuzungumza kuhusu shamba la mavuno kwa wale ambao bado hawajamjua, Yesu anakitambua chakula chake.

**Yesu alisema ni chakula kipi kinachomsaidia?**

Kufanya mapenzi ya Baba na kumaliza kazi aliyotumwa kuifanya. Kama ilivyo katika maswala ya kiasili, basi ni hivyo katika maswala ya kiroho kwa vile Mungu aliumba vitu vyote.

Kiroho, tunaposalimishwa kwa mapenzi ya Baba, tunapotumia muda wetu naye katika uwepo wake, katika ibaada, katika neno lake, kupokea kutoka kwake uzuri wake wote, kwa Roho wake, tutabadilishwa Zaidi na Zaidi kila siku.

**Wakati tunapokea kutoka kwa Yesu, kusalimishwa kwa mapenzi ya Mungu baba, tunabadilishwa kwa sura ya nani?** Soma **2 Wakorintho 3:17-18**

Yesu.

**Je Yesu anatangaza kwamba ni kitu gani kitakachofanyika iwapo tutakunywa Maji ya Uhai, kujisalimisha kwa mapenzi ya Baba?**

Soma **Yohana 15:8**

Tunda ni hakikisho. Kama ilivyo katika maswala ya kiasili, basi ni hivyo katika maswala ya kiroho kwa kuwa Mungu aliumba vitu vyote.

Wakati tunapojisalimisha kwa mapenzi ya Baba wetu na kunywa kila siku katikia uwepo wake, Roho Mtakatifu atatubadilisha tuwe Zaidi kama Yesu.  Tabia yake inakuwa tabia yetu.  Mti wa Yesu unatoa matunda ya Yesu.  Tunda la Roho.

**Ni tunda lipi la kiroho na hali ya kiundugu au tabia ya Yesu ambayo twapokea kutoka kwake, tunaposalimishwa kwa mapenzi ya Mungu Baba?** Soma **Wagalatia  5:22-23**

Upendo, furaha, amani, mateso ya muda mrefu, upole, uzuri, uaminifu, kujithibiti.

**Ni nani anayetengeza tunda?**

Mungu Baba, mwenye bustani, kupitia kwa Yesu Kristo Mwana, kwa Roho wake Mtakatifu. Tunapokuwa na ufunuo ya jinsi Mungu anavyotupenda, katika uwepo wake tumejisalimisha kwa mapenzi ya Baba, atajionyesha Zaidi kwetu kwa kuwa hayo ni mapenzi yake na tutajazwa na utimilifu wa Mungu.  Tunapokuwa katika uwepo wake kila siku, kupokea kutoka kwa Yesu, tumejisalimisha kwa mapenzi ya Baba, atatubadilisha, kwa kuwa haya ni mapenzi yake.

**Ni kitu gani kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu katika kipindi hiki?**

**Ni nini jibu lako au sala ya kweli?**

# Awamu ya 13: Mahusiano Kuwakubali wengine jinsi walivyo

*Kuwakubali wengine jinsi walivyo Maridhiano (leta katika hali ya kusikizana). Kurejeshwa (kurudisha kwa hali nzuri ya afya,). Kufanywa upya (kuamsha na kufanya iwe nzuri).*

## Sala ya Kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi,chagueni nyimbo mbili au tatu za ibaada ambazo zinatangaza upendo mkuu wa Mungu na nguvu za kubadilisha.

## Zoezi la Kundi la Mbegu Kumi

Kama vile tulijifunza, uhusiano wa muhimu ambao tunao ni uhusiano wa Mungu. Ikiwa tutasalimishwa kwa mapenzi ya Mungu na kutumia wakati naye, tukapokea mazuri yake yote, kila siku Mungu atatubadilsha tuwe na tabia ya Yesu Kristo.

Mungu anajali kuhusu hisia zetu, jinsi tunavyotendewa na wengine na jinsi tunavyowafanyia wengine.

## Zoezi la Kikundi

Kila mtu apaswa kuketi kwa mviringo huku wakiangaliana. Katikati ya mviringo, weka daftari la mbegu kumi (nakili kutoka ukurasa wa arobaini na tano wa Mwongozo wa Ufalme wa Mungu) ili kila mtu aweze kuona.

Kando ya daftari, weka mbegu kumi za mchele au mbaazi au mbegu yeyote ambayo yaweza kupatikana. Idadi ya watu katika mviringo ndio idadi ya kundi lako.Yaweza kuwa idadi ya watu kuanzia watatu hadi 12. Ikiwa ni Zaidi ya 12 tengeza vikundi viwili. Ikiwa Zaidi ya 24 tengeza vikundi vitatu na kadhalika.

Kila kundi lapaswa kuwa na mbegu 10 na daftari la mbegu 10 iwekwe katikati ya kundi. Kila mtu-mmoja mmoja-apaswa kupewa nafasi ya kuzungumzia kikundi. Kila mmoja ana sauti sawa. Kila mmoja ana umuhimu sawa. Kila mmoja ana umuhimu katika kikundi. Kila mmoja anatoa mawazo yake katika sehemu ya daftari jinsi wanavyohisi jamii inawatazama. Aidha jamii yao yawaona hawana umuhimu au jamii yao yawaona kuwa wenye umuhimu kiasi, au jamii yao yawaona wenye umuhimu mkubwa. Ni muhimu kwamba kila mtu aelewe kwamba hamna aibu kwa mtu kuhusu jinsi jamii inavyomtazama. Jinsi ambavyo jamii inamwona mtu yatokana na mambo mengi, ambayo mtu huyo hawezi kuyathibiti. Jibu mwafaka ni hili: jinsi unavyoamini jamii inakutazama.

Baada ya kila mmoja kutoa maoni yake katika daftari(hamna aliye na thamana au thamani kuu) kuhusu jinsi ambavyo jamii yawatazama, kila mmoja katika kundi ajadili jinsi ya kuyasema maoni ya kundi lao kwa kuweka mbegu kumi katika sehemu zilizotengwa. Mbegu zote kumi zapaswa kutumiwa. Mbegu hizo kumi zawakilisha kundi lote kwa ujumla.

Mfano wa 1: Ikiwa katika kundi la watu wanane, watano wahisi kwamba jamii haiwaoni kama watu wa thamana na watu wawili waamini kwamba jamii yawathamini, na mtu aamini kwamba jamii yawaona kama watu wa thamana kuu, basi mbegu 10 zitawekwa kama mbegu 7 katika nafasi ya kukosa thamani, mbegu 2 katika nafasi ya thamani Fulani na mbegu 1 katika nafasi ya thamani kuu.

Mfano wa 2: Ikiwa katika kundi la watu 6, watu 3 wahisi kwamba jamii haiwathamini, na watu 3 waaamini kwamba jamii yawaona kama watu wa thamani fulani, na hamna mtu anayewaona kama watu wa thamani kuu, basi mbegu 10 zitawekwa kama 5 katika sehemu ya hamna thamani, 5 katika sehemu ya thamani kiasi na sufuri (0) itakayowekwa katika sehemu ya thamani kuu.

## Mjadala wa Kikundi

Jadili mambo uliyoyaona. Andika majibu katika madaftari zenu.

**Twawezaje kuwafanya wale wanaoamini kwamba jamii yawaona kama watu wasio na thamani na pia thamani kiasi kuamini kwamba jamii yawaona kama watu wa thamani kuu?**

1. Wape heshima, jadili na hao kwa usawa, na uwajumuishe katika jamii.
2. Wapatie nafasi, jukumu, nafasi ya kushiriki katika jamii.
3. Wapatie nafasi ya kuzungumza na kuwa na maoni ya kushuhudia ukuu wa Mungu katika Maisha yao.
4. Wape nafasi ya kuzungumza, kuwa na maoni na sauti sawa.
5. Wapatie fursa ya kujua and kushuhudia ukuu wa Mungu, jinis ya kujitambulisha, karama na thamana yao.
6. Kila mmoja awe na fursa ya kutambua vi/kipawa chake ( kila mtu ana kipawa hata kama ni kimoja) na kutumia kipawa hicho kuwafaidi wengine.

## Somo la Bibilia

Soma **Luka 8:43-55**

## Muktadha

Katika kifungu hiki cha maandiko, mwanamke aliyefukuzwa kwao anafanya kila awezalo kumgusa Yesu. Katika tamaduni yake, angeonekana kuwa mtu mchafu na Yesu angechukuliwa kama mtu msafi.

## Mjadala wa Kikundi

Ni kitu kipi kilichofanyika kwa mwanamke huyu aliyefukuzwa kwao baada ya kumgusa Yesu katika **mistari ya 43-44?** Aliponywa (kimwili).

**Yesu alisema nini katika mstari wa 45?**

Ni nani aliyenigusa?

Yesu hakusema, ni kitu gani kilichonigusa bali NANI. Nani yamaanisha mwanadamu. Yesu anamthamini na anampa heshima kwa kutaka kumjua, anampatia muda wake na umakini wake. Tayari amepokea nguvu zake za uponyaji. Kumbuka kwamba Yesu yuko njiani kuenda kumwokoa msichana ambaye alikuwa anakufa,mtoto wa mtu wa hadhi katika macho ya ulimwengu.

**Mwanamike huyo alifanya nini katika mstari wa 47?**

Mwanamke huyo aliona kwamba hangeweza kujificha,alikuja mbele na akasujudia mbele ya Yesu na akashuhudia kwamba kwa mguso mmoja kutoka kwa Yesu, alipona.

Yesu hajamkubali tu mwanamke huyu aliyekataliwa kama mtu wa thamani ya juu, aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu Mkuu, bali kwa mguso mmoja kutoka kwa Yesu, jamii nzima, wanafunzi na Yesu mwenyewe wanamsikiza mwanamke huyu.

Ana nafasi. Ana sauti. Na ni mtu wa thamani. Yeye ni wa umuhimu.

**Yesu anamwita aje mbele ya wanafunzi wake na jamii yote katika mstari wa 48?**

Binti au mwana wa Mungu.

Mguso mmoja kutoka kwa Yesu wakamilisha kila kitu kimwili, kimawazo na kiroho. Ana nafasi, ana sauti, na anatambuliwa kwake kumerejeshwa kama mwana wa Mungu.

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu katika kipindi hiki?**

**Ni nini jibu lako au sala ya kweli?**

# Awamu ya 14: Mahusiano – Kuwa sawa

*'Mahusiano yaliyofunzwa yamerejeshwa kwa sawa-sawa katika Yesu...Ujumbe huu wahitajika sana kwa waliofikiwa na wale ambao hawajafikiwa….jamii nzima.' Mjumbe wa kongamano*

## Sala ya Kufungua

Muulize mtu afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni na muimbe nyimbo mbili au tatu za inaada ambazo zinatangaza upendo wa Mungu na nguvu zake za uponyaji.

Tutajifunza baadhi ya maswala ya jinsi ambavyo Mungu humchukulia mwanaume na mwanamke kuwa sawa-sawa kutoka kwa Hadithi yake, hadithi yake ya kweli ya upendo, Bibilia.

**Ili kuelewa mahusiano katika Ufalme wa Mungu kuishi katika ulimwengu ulioharibiwa na maovu, twapaswa kurudi hadi mwanzo.** Soma **Mwanzo 1:27-28**

Ni nzuri sana.

**Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wa nani?**

Mfano wa Mungu mwenyewe

**Mungu alimuumba mwanamke kwa mfano wa nani?**

Mfano wa Mungu mwenyewe

**Ni nani ambao Mungu aliwabariki kwa usawa?**

Mwanaume na mwanamke

**Ni nani ambao Mungu aliwapa uwezo wa kuutawala kwa usawa (mamlaka ya kutawala) ulimwengu wote?**

Mwanaume na mwanamke

Soma **Mwanzo 2:18-20**

Katika mstari huu, Mungu anamchukulia mwanamke kama msaidizi anayeweza kulinganishwa na mwanaume. Hii yamaanisha mtu wa kuja karibu, mtu wa mwili mmoja ilhali ni tofauti. Mtu aliye sawa na mwanaume, ambao kwa pamoja, waweza kuwa kitu kimoja. Mtu anayemkamilisha mwanaume kama aliyeumbwa katika mfano wa Mungu.

Katika Agano la Kale la Neno la Mungu, neno msaidizi mara nyingi latumiwa kumaanisha Mungu kuja karibu na mwanadamu. Katika Agano Jipya la neno la Mungu, Yesu anaashiria Roho wa Mungu au uwepo kama msaidizi wetu.

**Je Mungu alimuumba mwanaume na mwanamke sawa au la?**

Aliwaumba sawa

Mwanaume na mwanamke ni ustadi wa Mungu katika maumbili yote. Mwanadamu (mume na mke) walipokea pumzi ya Mungu, ya kutoshana, kusaidiana na kuwa na uhusiano wa usawa na Muumba Mungu na kila mmoja. Mwanaume na mwanamke **WALIUMBWA KWA MAZURI** ... sawa-sawa.



**WALIUMBWA KWA MAZURI**

**Je ulimwengu wa leo umekamilika?**

La

Jambo lilifanyika kubadilisha ulimwengu kamili wa Mungu. Kumbuka kwamba Mungu alimpa mwanamke na mwanaume uwezo wa kutawala ulimwengu wote na haki ya kutunza ulimwengu kamili wa Mungu.  Aliwapa kila kitu ili waishi kwa ushindi pamoja naye.

Mungu alimuumba mwanaume na mwanamke na uhuru wa kuchagua uzima au mauti, kuchagua kushiriki katika hekima ya Mungu na mti wa uzima, au kuchagua kushiriki uongo wa yule muovu na mti wa ufahamu wa mazuri na maovu.

**Ni chaguo lipi ambalo Mungu alimpatia mwanadamu (mwanaume na mwanamke)?** Soma **Mwanzo 2:8-9 na Mwanzo 2:15-17**

Uzima na mauti

Kabla ya mwisho wa sura ya tatu ya kitabu cha Ufunuo, mwanaume na mwanamke wa kwanza walichagua kushiriki uongo wa yule muovu na mti wa ufahamu wa mazuri na mabaya.  Hii ilikuwa badala ya kushiriki katika hekima ya Mungu na mti wa uzima.  Wote walichagua uhusiano wa kutokuwa waaminifu, umbali na kukataa hekima ya Mungu iliyosababisha kifo na uharibifu, badala ya uhusiano wa uaminifu, upendo na kupokea hekima ya Mungu ambayo in gesababisha uzima na kuzaa matunda.  Mwanaume na mwanamke waliruhusu kifo na maovu kuingia katika ulimwengu kamili wa Mungu. Soma **Mwanzo 3:1-7** na  **Mwanzo 3:16-17**

**Kwa sasa, uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke ukoje?  sawa au siyo sawa?**

Siyo sawa

Kila mmoja anataka kuthibiti na kuwa na mamlaka. Mwanamke anataka kumthibiti mwanaume na mwanaume anajaribu kumtawala mwanamke.

Soma  **Mwanzo 4:7**

Neno hamu katika muktadha huu katika **Mwanzo 3:16-17** lamaanisha

kukimbilia na kujaribu kuthibiti na kudanganya. Neno kutawala katika

muktadha huu wa  **Mwanzo 3:16-17** lamaan-isha kutawala na kukandamiza.

**Ni kitu gani ambacho mwanamke aliyeharibiwa na uovu anataka kumtendea mwanaume?**

Kumfuata na kujaribu kumthibiti na kumtawala

**Ni kitu gani ambacho mwanaume aliyeharibiwa na uovu aweza kumtendea mwanamke?**



WAMEHARIBIWA NA UOVU

Kutawala na kukandamiza.

Mwanaume na mwanamke **WAMEHARIBIWA NA UOVU**…..
Siyo sawa..Siyo sawa

Bali hadithi bado haiishi hapo.  Mungu katika upendo wake mkuu alishuka chini kwa maumbile yake kama mwanadamu wa mwili na damu na katika msalaba, alijichukulia hasara yote, ugonjwa, kifo na maovu ambayo yaliingia katika ulimwengu huu kutokana na makosa ya mwanadamu, Yesu alifufuka, akashinda hasara, magonjwa, kifo na maovu yote na ameturejesha kwa mazuri.



WAMEREJESHWA KWA UBORA

Mwanaume na mwanamke **WAMEREJESHWA KWA UBORA**…
sawa..sawa

Bali hadithi bado haishii hapo.  Mungu katika upendo wake mkuu anatupa nguvu na mamlaka yake kujua ukweli ili tusidanganywe. Tumepewa nguvu za kulaani uongo wa yule muovu na kuishi katika ushindi dhidi ya matakwa yetu ya kibinafsi katika ulimwengu huu ulioharibiwa na uovu.

Tunaposalimisha tamaa zetu za kutaka kuthibiti na kujitawala wenyewe na wengine kwa mapenzi ya Baba yetu na  tupokee yote kwamba Yesu alikuja

kama mwili na damu, akafa, akafufuka na akapaa juu ili atupe, nguvu za dhambi dhidi yetu inavunjwa.  Tunaishi kwa ushindi katika ulimwengu ulioharibiwa na uovu.  Mungu katika upendo wake mkuu atupa sehemu ya lengo lake la urejesho na uponyaji. Katika kipindi cha 15 na 16, tutajifunza upendo wa Mungu na sehemu anayotupa katika lengo lake la uponyaji, kutoka kwa hadithi yake ya upendo Bibilia.



WAMETUMWA KUPONYA

Mwanaume na mwanamke **WAMETUMWA KUPONYA**…sawa….sawa

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu katika kipindi hiki?**

**Ni nini jibu lako au sala ya kweli?**

# Awamu ya 15: Mahusiano – Uanafunzi

*Tunapoendelea na safari ya maisha, haijalishi ni hali gani ambayo tuko ndani, haijalishi ni wapi tunaenda, Yule mkuu yuko nasi….kwa ukaribu na kibinafsi.*

## Sala ya kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi,chagua na muimbe nyimbo mbili au tatu ambazo zinatangaza kwamba Mungu yuko nasi.

## Somo la Bibilia

Uanafunzi huanza kwa kumjua Mungu na upendo wake kwako, kwa kujua yeye ni nani, kile ambacho amefanya na atakachokifanya. Kuwa na wakati katika uwepo wake, kusikiza au kusoma neno lake, katika ibaada, katika maombi na katika ushirika na waumini wengine hutusaidia kumjua Mungu. Uanafunzi ndani yetu na kwa wengine ni jambo linaloendelea kila siku.

Kama vile tulivyojifunza katika kipindi cha uhusiano wa mzabibu, kubadilika kwa tabia na kukua kwetu ni kazi ya Roho Mtakatifu. Mungu hana haja na sisi kumtambua kwa wengine, bali kutokana na upendo wake mkuu kwetu, amechagua kuwa sehemu ya mpango wake. Kwa wengine kumjua Mungu, ukweli wake, upendo na nguvu, kwanza sharti wajifunze kumhusu .

**Sisi ni wanafunzi wa nani?**

Yesu

**Ni nani aliye na nguvu na mamlaka yote? Soma Mathayo 28:18-20**

Yesu

**Ni mambo yapi manne ambayo Yesu aliwambia wanafunzi wake wafanye katika mistari hii mitatu?**

1: Nenda

Katika muktadha huu, Nenda yaweza kumaanisha tunapoendelea katika Maisha(haijalishi hali ambayo tuko ndani), tunapotoka sehemu moja hadi nyingine(haijalishi tuko sehemu gani), Yesu ana nguvu na mamlaka yote katika hali hiyo na juu ya kila sehemu. Popote pale ambapo kila mmoja wetu yuko katika safari yake ya kila siku naye, Yeye yuko hapo, kwa undani na kibinafsi, katika Roho wake kwa kila mwanafunzi.

2: Kubatiza

Katika muktadha huu, kubatiza yamaanisha kuweka ndani au kuingiza ndani mara kwa mara, kusafisha, kuwa katika umoja na Yesu na kutambuliwa kwake. Kuwa naye katika kifo chake na ufufuo. Kumpokea Yesu ni kupokea kitambulisho chake, Roho wake na Baba. Kuingia kabisa

ndani yake ni kupokea nguvu zake na mamlaka, na kupitia kwa  hali ya moyo na akili kujisalimisha, kwa Roho wake, mabadiliko ya kudumu kwa wakati huu na wa siku za usoni.

3: Mafunzo

Mafunzo kamili ni kuwapa wengine uwezo wa kujifunza kumhusu Yesu, kukua katika uhusiano wao naye na kuwafunza wengine.  Kufunza sio kuwaonyesha wengine jinsi twajua mengi au kuonyesha kwamba sisi tuko sawa.  Kufunza katika muktadha wa kuwafanya wanafunzi wa Yesu ni kuwafunza wengine kutoka kila kabila, wanaume kwa wanawake (sawa-sawa), mtu mzima na mtoto (sawa-sawa) kuwa ndani ya Mungu, na kumtegemea kikamilifu.

4: Kuwafanya Wanafunzi

Katika muktadha huu kuwafanya wanafunzi ndilo lengo kuu. Twawafanya wanafunzi kwa kuwabatiza ili wawe ndani yake,kuwafunza kuwa watu wanaoweza kuwajibika kwa ukweli wake na kuwa maajenti wa lengo lake.

Lengo la Mungu wa kutimiza mpango wake **(Waefeso 1:9-10)**. Kuwafanya wanafunzi ni kazi ya Roho Mtakatifu na kupitia kwa wanafunzi wake.  Mungu amedhihirisha mpango wake kwetu sisi, wanafunzi wake na kwa sababu ya upendo wake mkuu kwetu ametupa kila mmoja wetu sehemu katika mpango wake.

Tunapojifunza kumhusu Yesu, tunapomjua Yesu kwa ukaribu siku baada ya nyingine katika uhusiano naye na kuwajua wale ambao tuko nao katika safari ya maisha, huku Yesu akishiriki nasi, twawaambia wengine kumhusu Yesu, tunapomruhusu Yesu kututumikia, tunamtumikia Yesu kwa kuwatumikia wengine, kwa Roho wake, katika jina lake, mpango wa Mungu unatimizwa.

Kila mwanafunzi ana Roho Mtakatifu ndani yake, ambaye ni shahidi wa Yesu. Ushahidi wako ni kuwa mtu ambaye Mungu alikuumba kuwa, kwa nguvu za kubadili za Yesu zilizo ndani yako. Kila mwanafunzi ana ushuhuda ambao ni shahidi wa Yesu.




## Ushuhuda

**Ulikuwa mtu wa aina gani kabla ya kuwa mwanafunzi wa Yesu?**

**Wewe ni mtu wa aina gani kama mwanafunzi wa Yesu anayeonyesha utofauti ambao Yesu ameufanya?**

**Maisha yako yalikuwa ya aina gani ulipoamua kumpokea Yesu na kuwa mwanafunzi wake?**

**Ni kitu gani cha maana ambacho kilikufanya umpokee Yesu na kuwa mwanafunzi wake?**

**Ni utofauti upi wa maana katika maisha yako sasa na wa siku zijazo?**

Kila mtu mmoja mmoja aweze kutoa ushuhuda wake (na usiwe Zaidi ya dakika mbili) kana kwamba anamwambia mtu ambaye sio mkristo.  Jiepushe kutumia maneno kama haki na wokovu, badala yake eleza maana ya wokovu maishani mwako.

**Ni nini jibu lako au sala ya kweli?**

# Awamu ya  16: Mahusiano - Ufalme wa Mungu

Tunakuwa mfano wa yule tunayemwabudu.

## Maombi ya Kufungua

Muulize mtu mmoja afungue kikao kwa maombi.

## Ibaada

Kama kikundi, chagueni na muimbe wimbo mmoja au mbili za ibaada zinazotangaza Yesu ni Mfalme!

Kumbuka kwamba katika mwanzo wa safari hii pamoja,tulijifunza kwamba Mungu anataka kujitambulisha na mpango wake, ambao ni kuleta vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani pamoja katika Kristo Yesu.

## Somo la Neno

Ufalme wamaanisha haki au mamlaka au uwezo wa kutawala juu ya ufalme na sehemu au mahali palipo chini ya utawala huo.

Mungu yamaanisha kitu kitakatifu ambaye twamjua kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Ufalme wa Mungu ni haki au mamlaka au nguvu za Yesu kutawala mbinguni na ulimwengu. Yesu  ni mtawala wa Ufalme wa Mungu.  Katika awamu ya 10 Kuzaliwa kwa Roho tulijifunza kwamba ili kuingia katika Ufalme wa Mungu ni sharti tumpokee Mfalme.  Taswira ya Ufalme wa Mungu ni muhimu kuelewa ujumbe na  huduma ya Yesu Kristo na jukumu la wanafunzi wake katika lengo lake la uponyaji.

## Somo la Bibilia

Soma **Luka 4:43** na  Matendo ya **Mitume 1:1-4**

Yesu alihubiri na kufunza kuhusu Ufalme wa Mungu, akaonyesha Ufalme wa Mungu, naye ni mtawala wa Ufalme wa Mungu.

Yesu alisema ni kitu gani kinachotimizwa kwa kuja kwake kimwili na damu? Soma **Luka 4:18-19**

1. Kuwahubiria maskini habari njema.
2. Waponye waliovunjika mioyo
3. Uhuru kwa walio mateka
4. Vipofu wapate uwezo wa kuona
5. Uhuru kwa waliokandamizwa
6. Tangaza kwamba huu ndio mwanzo wa wakati wa Mungu ambapo mambo haya yatafanyika.

Ufalme wa Mungu umekuja ulimwenguni kwa Yesu Kristo, katika ulimwengu ulioharibiwa na uovu.

**Ni kitu gani ambacho Yesu alimwambia Yohana kuwa ushahidi kwamba Ufalme wa Mungu/ Ufalme wa Mbinguni ulikuwa umekuja duniani?** Soma **Mathayo 11:3-5**

1: Vipofu waone

2: Viwete watembea

3: Walio wachafu wasafishwe

4: Viziwi wasikia

5: Waliokufa wafufuliwa

6: Maskini watangaziwa injili

Katika Agano la Kale kuna unabii mwingi ambapo vipofu wataona, viwete watembea na viziwi watasikia. Hii haimaanishi tu uponyaji wa kiroho. Yesu alitambua Ufalme wa Mungu ni uponyaji kamili; kiroho, kimwili na kimawazo. Ukamilifu wote na Amani.

Mungu Baba alimtuma Yesu katika ulimwengu ulioharibiwa na uovu(ambao uko chini ya uwezo wa yule muovu na tamaa za mwanadamu za kutaka kutawala na kudhibiti) kuwaweka huru waliotekwa, kuwaponya waliovunjika mioyo na kutangaza kwamba Ufalme wa Mungu umefika. Wanaoamini na kupokea dhabihu ya mwili na damu ya Yesu mwenyewe wanaokolewa milele na milele. Wameokolewa kutoka kwa ufalme wa mauti na kuletwa kwa Ufalme wa Uzima.

Soma **Mathayo 19:13-15** (Pia **Marko 10:13-16** na **Luka 18:15-17**).

**Twajifunza nini kuhusu mtazamo wa Yesu kwa watoto?**

Hata ingawa Yesu alifananisha Imani ya mtot kwa Ufalme wa Mungu, ile hali ya Yesu kuwahubiria watoto ni muhimu sana na imejumlishwa katika Injili zote tatu. Utamaduni wa muda, katika ulimwengu huu ulioharibiwa na uovu ulikuwa kwamba, watoto walikuwa na thamana ya chini kuwaliko watu wazima. Wanafunzi walikuwa wanafuata utamaduni wa ulimwengu huu na wala hawakuwa wanaishi katika utamaduni wa Ufalme wa Mungu. Kwa matendo yake, Yesu alikuwa anahubiri na kuwaonyesha wanafunzi wake jinsi ambavyo Ufalme wa Mungu unavyofanana katika ulimwengu ulioharibiwa na uovu.

**Je, Yesu auchukulia namna gani uhusiano wa watoto na watu wazima, sawa au siyo sawa?**

Sawa

## Mjadala wa Kikundi

Jadilieni kama kikundi Ufalme wa Mungu ni nini?

1: Mahusiano yaliyorejeshwa na Mungu na wen-gine, mwanaume, mwanamke, kijana, msichana….sawa-sawa

2: Masikini na tajiri wanakuwa na nguvu….sawa-sawa

3: Jamii ya waliotoshana ikijengana kwa pamoja

4: Kujumuishwa kwa watu wote wanaomwamini na kuishi katika Yesu

5: Kujenga jamii yenye haki na amani

6: Waliotekwa nyara wawekwa huru na ukweli na upendo

7: Matendo ya kweli yanakuwa mwenendo.

Ufalme wa Mungu umedhihirishwa katika Yesu.

Yesu ametukabidhi, kwa Roho wake, katika nguvu na mamlaka yake, kuishi katika Ufalme wa Mungu ndani ya ulimwengu huu ulioharibiwa na uovu na kuwa sehemu ya mpango wa Mungu kwa ufalme wake, kwa utukufu wa Mungu Baba.

Tunapoendelea kumjua Mungu zaidi na upendo wake kwetu, kuwa Naye katika uwepo wake, kusikiza au kulisoma Neno lake, katika ibaada, katika maombi, katika ushirika na waumini wengine, kupokea kutoka kwa Yesu, kuishi katika ukuu wa ushindi wake katika ulimwengu huu ulioharibiwa na uovu, kushuhudia upendo wake mkuu na kuwafanya wanafunzi, twaishi ndani ya Ufalme wa Mungu hapa duniani na kwa wakati huu.

**Ni kitu kipi kimoja ambacho umejifunza kumhusu Mungu katika kipindi hiki?**

**Ni nini majibu yako mwafaka/maombi?**

## Maombi

*Waefeso 3:14-21 Kwa sababu hii nampigia Baba magoti, ambaye kwa Yeye ubaba wote wa kila jamaa za mbinguni na za duniani unaitwa. Kwa sababu hii nampigia Baba magoti, 15ambaye kwa Yeye ubaba wote wa kila jamaa za mbinguni na za duniani unaitwa. Namwomba Mungu awaimarishe kwa kuwatia nguvu mioyo yenu kwa njia ya Roho Wake kwa kadri ya utajiri wa utukufu Wake, ili kwamba, Kristo apate kukaa mioyoni mwenu kwa njia ya imani. Nami ninaomba kwamba ninyi mkiwa wenye mizizi tena imara katika upendo, muwe na uwezo wa kufahamu pamoja na watakatifu jinsi ulivyo upana na urefu na kimo na kina upendo wa Kristo na kujua upendo huu kwamba unapita fahamu, ili mpate kujazwa na kufikia kipimo cha ukamilifu wa Mungu. Basi kwa Yeye awezaye kutenda mambo ya ajabu yasiyopimika kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya uweza Wake ule utendao kazi ndani yetu, Yeye atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu kwa vizazi vyote, milele na milele. Amina.*

| Hakuna thamani | Thamani Kidogo | Thamani Kubwa |
| --- | --- | --- |
| | | |